KUCHUNGUZA MCHANGO WA MAZINGIRA YA KIMAUMBILE KATIKA KUIBUA MAJINA YA MAHALI KISIWANI PEMBA

BIMKUBWA ABDULLA HAMZA

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUKAMILISHA SEHEMU YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI (M A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

ITHIBATI

Nathbitisha kwamba, aliyesaini hapo chini ameisoma tasnifu hii Kuchunguza **“Mchango wa Mazingira ya Kimaumbile katika Kuibua Majina ya Mahali Kisiwani Pemba”** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunikiwa Degree ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…….…….

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

Tarehe….……..……..

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki, kwa namna yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi ***Bimkubwa Abdulla Hamza*** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yeyote.

……

Saini

Tarehe……..

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa; Marehemu bwana Abdulla Hamza na bi Fatma Mohammed Hamad. Nawashukuru wawili hawa kwa kuniongoza vyema katika maisha na kunisomesha mpaka nikafikia hapa nilipo. Pia naitunuku kazi hii kwa watoto wangu wapendwa; Mahmoud Sufiani Juma, Mahdi Sufiani Juma, Abdalla Sufiani Juma na Swafaa Sufiani Juma. Kazi hii iwe ni chachu kwao katika utafutaji wa elimu ili wafikie daraja za juu zaidi ya hapa nilipo mimi. Iwape nguvu ya kukumbuka kwamba elimu ndio msingi wa maisha. Mwisho kabisa naitunuku kazi hii kwa mume wangu mpenzi bwana Sufiani Juma Khamis kwa uvumilivu wake mkubwa katika kipindi chote cha kufanya utafiti na kuandika ripoti hii.

SHUKURANI

Awali ya yote na mshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa ulimwengu pamoja na viumbe vyote vya Ardhini na Mbinguni. Ni yeye Mola Mkwasi aliyenipa nafasi, nguvu, afya, uwezo na ujasiri hadi kukamilika kwa kazi hii. Baada ya shukurani kwa mola wetu mmoja, nachukuwa nafasi hii kuwashukuru wale wote walionisaidia kwa namna yoyote ile katika kufanikisha kazi hii. Najali na kuuthamini sana mchango na mashirikiano yao kwangu. Nakiri wazi wazi kwamba bila ya wao kazi hii ingekuwa ngumu kwangu kuikamilisha. Kutokana na wingi wao ni vigumu sana kuwataja na kuwaorodhesha hapa mmoja baada ya mwengine. Lakini natumia fursa hii kuwataja wachache ambao ni vigumu mno kuwasahau kutokana na mchango na umuhimu wao kwangu. Shukrani za pekee ziende kwa msimamizi wangu, Mwalimu Bakari Kombo Bakari, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu na kwa moyo wake wa kunihimiza kufanya kazi kila alipohisi kuwepo kwa uduwazi na namna fulani ya kusita na kucheleweshe kazi. Yeye alikuwa kwangu ni mshauri, muelekezaji na mwalimu aliyenikosoa kwa busara na hekima kubwa kila ilipobidi kukosolewa na kuelekezwa. Sina cha kumlipa, lakini sitoacha kumuombea dua kwa Mwenyeezi Mungu amzidishiye moyo wa upendo na ampe nguvu aweze kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kwa manufaa ya sasa na baadae, ili wanufaike wengi wa enzi hizi na zijazo. Sina budi pia kuwashukuru wazazi wangu, kaka na dada zangu wote kwani wao ndio msingi wa maisha yangu. Shukurani za pekee zimwendee mume wangu mpenzi bwana Sufiani Juma Khamis ambae alikuwa nami bega kwa bega katika kunishauri, kuniongoza na kunipa moyo katika masuala ya kielimu na hakuniacha mkono hadi alipohakikisha nafikia nilipo sasa. Shukurani maalumu ziwaendee watoto wangu wapendwa kwa uvumilivu wao waliouonesha hasa pale ilipobidi niwe

nao lakini walinikosa kutokana na harakati za kazi hii. Shukurani za dhati zimwendee msimamizi wangu ambae aliniongoza hadi kukamilika kwa tasnifu hii. Shukurani mahususi ziwendee wote waliofanikisha kupatikana kwa taarifa za utafiti huu. Mwisho nawashukuru wanachuo wenzangu kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha masomo.Nawatakia kila la kheri.Amiin.

IKISIRI

Kazi hii ilihusika na Kuchunguza Mchango wa Mazingira ya Kimaumbile katika Kuibua Majina ya Mahali Kisiwani Pemba**.** Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ambayo ni kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile yanayochangia upatikanaji wa majina ya mahali kisiwani Pemba na kuchunguza historia ya mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali kwenye sehemu mbalimbali katika kisiwa cha Pemba. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa mbinu mbalimbali za utafiti zilihusika, ambazo ni hojaji na mahojiano. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia jumuishi ya Giles ambayo msingi wake mkubwa ni kuchunguza vibainishi vya jamii mbalimbali. Sampuli iliyotumika ni watu themanini na moja (81), kutoka maeneo mbalimbali ya Pemba. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, aligundua kwamba mtafiti alibaini kuwa kisiwni Pemba yapo majina mengi yaliyotokana na mazingira ya kimaumbile kisiwni hapa. Mazingira ya kimaumbile yaliyochangia majina hayo ni miti mikubwa, milima, hali ya ardhi, mito, maziwa, shughuli za kibinaadamu kama mava, mabonde, mawe, na maumbile mengine. Kuhusu lengo la pili, mtafiti amegundua asili na historia ya majina hayo, na jinsi yalivyoibua majina ya mwahali humo. Alibaini shughuli kama uvuvi, usafiri, kilimo, ugomvi, mapumziko, uchotaji maji mitoni na pirika nyengine zilitoa umashuhuri wa mwahali humo na kufanya watu waamue kuyaita majina ya mahali kutegemeana na mazingira ya mahali hapo. Amebaini pia baadhi ya asili changizi zilizoibua majina zimetoweka na nyigine zinalindwa na kuhifadhiwa. Nyengine zimehifadhika kimaumbile na nyengine zimehifadhiwa kwa jitihada maalum za kijamii.

YALIYOMO

ITHIBATI i

HAKIMILIKI ii

TAMKO iii

TABARUKU iv

SHUKURANI v

IKISIRI … vii

YALIYOMO viii

ORODHA YA MAJEDWELI xiv

ORODHA YA PICHA xv

ORODHA YA VIFUPISHO xvi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Utafiti 1

1.3 Tatizo la Utafiti 2

1.4 Malengo ya Utafiti 3

1.4.1 Lengo la Jumla 3

1.4.2 Malengo Mahsusi 4

1.4.3 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Mipaka na Eneo la Utafiti 5

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA 6

2.1 Utangulizi 6

2.2 Kazi Tangulizi 6

2.3 Maana ya Mapitio ya kazi Tangulizi 6

2.4 Mapitio kuhusu Majina na Aina zake 7

2.5 Kazi Tangulizi zinazohusu Majina ya Mahali 9

2.6 Mkabala wa Kinadharia 13

2.7 Hitimisho 14

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 15

3.1 Utangulizi 15

3.2 Mpango wa Utafiti 15

3.3 Kundi Lengwa 16

3.4 Eneo la Utafiti 16

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji 17

3.4.2 Mbinu za Kukusanya Data 19

3.4.3 Hojaji 19

3.4.4 Mahojiano 20

3.5 Maadili ya Utafiti 20

3.6 Hitimisho 21

SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 22

4.1 Utangulizi 22

4.2 Majina ya Mahali yaliyoibuka kutokana na Mazingira ya Kimaumbile..... 22

4.2.1 Kijiji cha Mivumo Ishirini 23

4.2.2 Kijiji cha Kidutani (Kidutani cha Bamkuja) 23

4.2.3 Kijiji cha Bubujiko..... 24

4.2.4 Kijiji cha Mtoni Msengele 24

4.2.5 Kijiji cha Jiweni 25

4.2.6 Kijiji chaNdaambani 25

4.2.7 Kijiji cha Mchangani..... 26

4.2.8 Kijiji cha Miti Ulaya 26

4.2.9 Kijiji cha Mawe Matatu 27

4.2.10 Kijiji cha Chanjamjawiri..... 27

4.2.11 Kijiji cha Kilimandege..... 28

4.2.12 Kijiji cha Minazini 28

4.2.13 Kijiji cha Tibirinzi/Kibirnzi 29

4.2.14 Kijiji cha Mtoni Chakechake 29

4.2.15 Kijiji cha Mbuyu Mkavu..... 30

4.2.16 Kijiji cha Mvumoni..... 31

4.2.17 Kijiji cha Mkungupigi..... 31

4.2.18 Kijiji cha Mavani Chaka la Kati 32

4.2.19 Kijiji cha Mikarafuu Giza 32

4.2. 20 Kijiji cha Mavapacha 32

4.2.21 Kijiji cha Mkoroshoni..... 33

4.2.22 Kijiji cha Miembeni..... 34

4.2.23 Kijiji cha Konde..... 34

4.2.24 Kijiji cha Mabaoni 35
4.2.25 Kijiji cha Uwandani 35
4.2.26 Kijiji cha Kijiwe Mtu 36
4.2.27 Kijiji cha Dumbini 36
4.2.28 Kijiji cha Msingini 37
4.2.29 Eneo la Mto Mkuu 37
4.2.30 Kijiji cha Ziwani 37
4.2.31 Kijiji cha Mtemani 38
4.2.32 Kijiji cha Misufini 38
4.2.33 Kijiji cha Ndagoni 39
4.2.34 Kijiji cha Miburani 39
4.2.35 Kijiji cha Michungwani 39
4.2.36 Kijiji cha Kichungwani 40
4.2.37 Kijiji cha Changaweni 41
4.2.38 Kijiji cha Vilima Vitatu 41
4.2.39 Kijiji cha Limani 41
4.2.40 Kijiji cha Bandari Kuu 42
4.2.41 Kijiji cha Vuma Wimbi 42
4.3 Historia za Kuibuka kwa Majina kutokana na Mazingira ya Kimaumbile 42
4.3.1 Historia ya Kijiji cha Mivumo Ishirini 43
4.3.2 Historia ya Kijiji cha Kidutani 43
4.3.3 Historia ya Kijiji cha Bubujiko 45
4.3.4 Historia ya Kijiji cha Mtoni Msengele 46

4.3.5 Historia ya Kijijij cha Jiweni 47

4.3.6 Historia ya Kijiji cha Ndaambani..... 48

4.3.7 Historia ya Kijiji cha Mchangani 49

4.3.8 Historia ya Kijiji cha Miti Ulaya..... 50

4.3.9 Historia ya Kijiji cha Mawe Matatu..... 51

4.3.10 Historia ya Kijiji cha Chanjamjawiri 52

4.3.11 Historia ya Kijiji cha Kilimandege 54

4.3.12 Historia ya Kijiji cha Minazini..... 55

4.3.13 Historia ya kijiji cha Tibirinzi..... 56

4.3.14 Historia ya Kijij cha Mtoni Chake chake..... 57

4.3.15 Historia ya Mbuyu Mkavu 58

4.3.16 Historia ya Kijiji cha Mvumoni 59

4.3.17 Historia ya Kijiji cha Mkungupigi 59

4.3.18 Historia ya Kijiji cha Chaka la Kati 60

4.3.19 Historia ya Kijiji cha Mikarafuu Giza..... 61

4.3.20 Historian ya Kijiji cha Mavapacha..... 61

4.3..21 Historia ya Kijiji cha Mkoroshoni 62

4.3.22 Historia ya Kijiji cha Miembeni..... 63

4.3.23 Historia ya Kijiji cha Konde 64

4.3.24 Historia ya Kijiji cha Mabaoni..... 64

4.3.25 Historia ya Kijiji cha Uwandani..... 65

4.3.26 Historia ya Kijiji cha Kijiwe Mtu 66

2.3.27 Historia ya Kijiji cha Dumbini..... 67

4.3.28 Historia ya Kijiji cha Msingini 67

4.3.29 Historia ya Eneo la Mto Mkuu 68
4.3.30 Historia ya Kijiji cha Ziwani 69
4.3.31 Historia ya Kijiji ncha Mtemani 69
4.3.32 Historia yaKijiji cha Misufini 70
4.3.33 Historia ya Kijiji cha Ndagoni 71
4.3.34 Historia yaKijiji cha Miburani 71
4.3.35 Historia ya Kijiji cha Michungwani 72
4.3.36 Histioria ya Kijiji cha Kichungwani 73
4.3.37 Historia yaKijiji cha Changaweni 74
4.3.38 8Historia ya Kijiji cha Vilima Vitatu 74
4.3.39 Historia ya Kijiji cha Limani 75
4.3.40 Historia ya Kijiji cha Bandari Kuu 75
4.3.41 Historia ya Eneo la Vuma Wimbi 76

SURA YA TANO: MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NAMAPENDEKEZO 78

5.1 Utangulizi 78
5.2 Muhutasari 78
5.3 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti 79
5.4 Hitimisho 80
5.4.1 Mapendekezo ya Tafiti 80

MAREJELEO 81

VIAMBATANISHO 86

ORODHA YA MAJEDWELI

Jedwali Na.3.1: Makundiya Watafitiwa, Maeneo watokayo na Idadi yao 18

ORODHA YA PICHA

Picha 4.11: Inayoonesha Chanjaa la Mjawiri lilivyokuwa hapo awali kabla ya kuwa makaazi ya watu. (Chanzo cha picha hii ni makumbusho ya Utamaduni-Pemba). 54

ORODHA YA VIFUPISHO

VIFUPISHO

TUKI	Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili
BAKIZA	Baraza la Kiswahili Zanzibar

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa na shabaha ya kuchunguza mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali kisiwani Pemba. Sura hii kwa ujumla ina shabaha ya kubainisha na kuvifafanua kwa ufupi vipengele vya kiutangulizi vinavyohusu utafiti huu. Miongoni mwa vipengele hivyo ni usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambayo yanahusisha lengo la jumla pamoja na malengo mahususi. Maswali ya utafiti pia yamebainishwa katika eneo hili. Vipengele vingine vilivyojadiliwa ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na eneo la utafiti.

1.2 Usuli wa Utafiti

Majina ni mojawapo ya kategoria ya maneno ambayo imewahi kushughulikiwa na wataalamu kadha. Baadhi ya wataalamu hao ni Mgullu (1999), Massamba (2004), Matinde (2012), Saluhaya (2010), Kihore na wenzake (2008). Kihore na wenzake (weshatajwa) kwa mfano, wameeleza kuwa jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa au tukio katika tungo. Ally na wenzake (1930) kwa upande wao wamefafanua kwamba jina ni kila analoitwa mwanadamu, mnyama, mmea, vitu vigumu au kitu kingine chochote. Fasili ya jina kwa mujibu wa utafiti huu ni neno linalotaja vitu, viumbe, hisia au hali ili kuvitofautisha na vitu vyengine. Kihore (2009) ameainisha aina za majina kuwa ni majina jumuishi, majina ya pekee na majina ya kikundi. Pia Kihore (keshatajwa) ameainisha kuwepo kwa majina ya kawaida kama vile kiti, daftari, kalamu. Majina

ya pekeeni yale ambayo huwa na umbo na tabia ya kipekee au mahususi. Majina ya aina hii ni yale wanayoitwa watu na mahali. Mfano wa majina ya watu ni kama vile, Ahmad, John, Khamisi; majina ya mahali mifano yake ni kama vile, Shengejuu, Konde, Jadida, Uwandani, Bahanasa, n.k. Ni kweli kwamba John wanaweza kuweko wengi duniani lakini bila shaka kila mmoja anatofautiana kabisa na John mwengine .Tofauti zao zinajitokeza katika maumbo na tabia zao. Jina la mahali panapoitwa Kianga kwa mfano linapatikana Unguja kwa upande mmoja na Pemba kwa upande wa pili ni Kianga mbili zinazotofautiana kimazingira yawezekana na asili yake pia.

Kama tulivyobainisha hapo juu (1.0), Majina ya mahali ni aina mojawapo ya majina ya pekee. Majina haya kwa desturi hutaja miji, vijiji, mitaa, vitongoji, na maeneo yenye historia fulani .Majina ya mahali ni miongoni mwa maneno yanayotumiwa na wanajamii katika shughuli zao za kila siku ni kipengele chenye umuhimu mkubwa kwa wanajamii kwani hutambulisha utamaduni wao, kujua historia yao na kujua maana yaliyomo ndani ya majina. Mtafiti katika kazi hii amenuia kuchunguza“mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahala kisiwani Pemba.” Kwa kuchunguza historia ya majina ya mahali yanayopatikana kisiwani Pemba.

1.3 Tatizo la Utafiti

Suala la majina ya mahali limetafitiwa na wataalamu mbali mbali wa nje na ndani ya Tanzania. Tafiti nyingi zinaonyesha na kuashiria kuwa kuna mambo mengi yanayochangia mahali fulani kupewa jina fulani. Miongoni mwa sababu hizo ni za kijamii, shughuli za kisiasa pamoja na mila na utamaduni. Mlacha (1995), anadai kuwa jina la mahali panapoitwa Uvuani limetokana na utamaduni wa kazi ya uvuvi.

Mlacha (keshatajwa) anaongezea kuwa majina ya mahali ya Waswahili yanaakisi kumbukumbu za yaliyopita yanayohusiana na mambo ya kisiasa au maswali ya kijamii. Vilevile, Salim (1984) anaelezea kuwa majina ya mahali kama kama Ndagoni, yametokana na maingiliano ya wageni na wenyeji wa Asia na India. Anaongeza kuwa majina kama Malindi, Kiwayu, Pemba na Uziwa yana asili ya Uswahili na yanaeleza historia na utamduni ya Waswahili wa mwambao. Zubeir (2015), alibaini kwamba majina ya mahali kisiwani Pemba yanaakisi moja kwa moja utamaduni wa Wapemba na shughuli walizokuwa wakifanya zilichangia vya kutosha kuibua majina ya mitaa na vijiji katika jamii hii.

Watafiti waliotangulia pamoja na kuchunguza majina ya mahali na asili zake katika jamii za Wapemba kupitia vigezo tofauti, lakini hata hivyo kwa kiwango anachoelewa mtafiti, tafiti zinazoelezea mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali Kisiwani Pemba bado haujafanywa". Kwa muktadha huo, mtafiti alishawishika kufanyia utafiti eneo hili, ili kugundua ni kwa kiasi gani ***mazingira ya kimaumbile*** yamechangia katika kuibuwa majina ya mahali na historia zilizopelekea kuibuka kwa majina hayo kisiwani Pemba.

1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawika katika lengo la jumla na malengo mahsusi.

1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahala kisiwani Pemba.

1.4.2 Malengo Mahsusi

i. Kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile kisiwani Pemba.

ii. kuchunguza historia ya mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali kwenye sehemu mbalimbali katika kisiwa cha Pemba.

1.4.3 Maswali ya Utafiti

i) Ni majina gani ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile kisiwani Pemba?

ii) Ni historia gani iliyopelekea kuibuka kwa majina ya mahali kulingana na mazingira yaliopo?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Baada ya kukamilka kwake utafiti huu unatazamiwa kuwa ni miongoni mwa marejeo ya kimaktaba yatakayowawezesha walimu, wanafunzi na wadau wengine wa kitaaluma kupata fursa ya kwenda kuusoma na kutambua baadhi ya mambo yanayohusiana na mahali tofauti pamoja na historia za maeneo hayo. Pili utafiti huu utakuwa ni kama marejeo ya kidarasa, yatakayowasaidia walimu katika kufundisha na wanafunzi katika kujifunza. Tatu, matarajio ya mtafiti ni kuwa utafiti huu utawashawishi wanaisimu wa kileo kufanya tafiti nyengine ambazo zitahusiana na maswali ya historia ya majina ya mahali hapa Pemba na kwenginepo duniani. Nne, kazi hii itakuwa na umuhiumu mkubwa kwa wanajamii wa Kipemba kwa kuwa itakuwa ni kumbukumbu inayoonesha ustawi miji, vijiji na mitaa yetu hapa kisiwani Pemba.

1.6 Mipaka na Eneo la Utafiti

Kijiografia utafiti huu unakusudia kufanyika katika eneo la Pemba na sio kwenye maeneo mengine ambayo mazingira ya kimaumbile yaliochangia katika kuibua majina ya mahali.

Kitaaluma historia za majina ya mahali zitachunguzwa lakini hata hivyo majina yatakayohusika na mambo megine hayatachunguzwa. Mtafiti atachunguza mazingira ya kimaumbile yanavyochangia kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba.Mtafiti amechagua Kisiwa cha Pemba kufanyia utafiti huu kwa sababu katika kupitia maandiko mbalimbali hakugundua maandishi yanayoelezea kuhusiana na mazingira ya kimaumbile yanavyochangia kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba. Mtafiti hatajishughulisha na majina yasiotokana na mazingira ya kimaumbile.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imeangazia na kuzungumzia maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Mtafiti alipitia kazi tangulizi ili kuona ni kwa namna gani watafiti na wataalamu mbalimbali walivyoandika kuhusu mada zenye ukaribu na utafiti huu. Vilevile mtafiti alieleza nadharia iliyoongoza utafiti huu.

2.2 Kazi Tangulizi

Kazi tangulizi ni mpangilio maalumu uliofafanuliwa na kuchambuliwa kimaandishi kuhusu habari inayohusiana na suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi yanapaswa yaoneshe uhusiano wa moja kwa moja na mada unayoifanyia utafiti.Hapa mtafiti hulazimika kupitia tafiti mbali mbali zilizowahi kufanywa ambazo zina uhusiano na mada inayotafitiwa. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi lazima yaoneshe ufafanuzi na mahitaji hususani, iwapo utafiti umewahi kufanywa hapo kabla unaohusu mada kama hiyo (Enon, 1998).

2.3 Maana ya Mapitio ya kazi Tangulizi

Pons (1992) alibainisha kuwa kupitia kazi tangulizi huhusisha kupitia nyaraka, usomaji wa machapisho yaliyoandikwa ambayo mtafiti hutegemea kuibua maarifa anayotafuta kulingana na mada na malengo yake ya utafiti.Mtafiti wa kazi hii ametalii machapisho mengi sana yakiwemo majarida, wavu pepe, tasnifu na hata vitabu. Mtafiti pia amesikiliza vyombo vya habari ili kupata data anazozihitaji. Pia, kutalii ni namna ya usomaji kwa lengo la kupekua taaluma iliyojificha. Kwa kulielewa hili, mtafiti alilazimika kusoma vitabu, majarida, tasnifu za watafiti

waliomtangulia, mitandao ili kufichua siri za watafiti tangulizi na kupata maarifa zaidi na wepesi wa kufanya utafiti huu.

2.4 Mapitio kuhusu Majina na Aina zake

Dhana ya majina ina upeo mkubwa, na imejadiliwa na wataalam wengi wa fani ya isimu.Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa mazingira ya kimaumbile jinsi yanavyochangia kuibua majina ya mahala kisiwani Pemba. Hivyo basi majina ya mahala yanayotokana na mazingira ya kimaumbile ndio ajenda kuu inayoangaliwa kwenye utafiti huu. Baadhi ya wataalam walioangalia kuhusu majina ni pamoja na Kihore na wenzake (2008), ambao wameeleza kwamba jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa, au tukio katika tungo. Katika sehemu hiyo, Kihore na wenzake (weshatajwa) wameainisha aina tatu za majina ambazo ni (1) Majina jumuishi ambayo pia huitwa majina ya kawaida. (2) Majina Mahsusi na (3) majina ya jamii ambayo pia huitwa majina ya kikundi.

Kapinga (1993) kwa upande wake ameainisha aina saba za majina, kama ilivyoorodheshwa na mtafiti hapo chini. 1) Majina ya pekee (2) Majina ya kawaida (3) Majina ya Dhahania (4) Majina ya mguso (5) Majina ya kitu kimoja kimoja (6) Majina ya jamii (7) Majina ya wingi. Mgullu (1999) ameainisha aina sita za nomino (1) nomino za pekee (2) nomino za kawaida (3) nomino za mguso (4) nomino za dhahania (5) nomino zinazohesabika na zisizo hesabika na (6) nomino za jamii .

Nyangwine na Masebo (2006) wameziainisha aina tano za nomino, ambazo ni (1) Nomino za pekee (2) Nomino za kawaida (3) Nomino za Dhahania (4) Nomino za jamii (5) Nomino za wingi. Tukichunguza tutagundua kuwa wataalam wote hawa, pamoja na kutofautiana kuhusu aina za majina wamekubaliana kuwepo kwa majina ya pekee ambayo sana huhusisha mahali na maumbile ya kijografia.

Kapinga (keshatajwa), ameelezakuwa majina ya pekee ni kama vile majina ya watu mfano: Khamis, Maria, Songambele, Taabu na mengi mengineyo. Majina ya mahali kwamfano, ni kama vile Tanga, Kilimanjaro. Majina ya siku kama Jumatatu, Jumanne, Jumatano na kadhalika pia yanaingia katika eneo hili. Majina ya miezi Januari, Februari, Marchi na kadhalika ni kipengele kinachohusu pia eneo hili.

Mgullu (keshatajwa) anasema”nomino za pekee ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee. Kitu cha pekee ni kitu mahsusi na ni cha pekee kwa sababu kina kuwa kipo chenyewe tu.Anaendelea kusema kuwa hapa duniani, nomino za pekee hutaja majina ya watu kama vile Juma, Omar, Tumaini na mengi mengineyo. Majina ya pekee pia hutaja majina ya miji kama vile Nairobi, Dodoma na miji mingineyo. Majina ya nchi kama vile Kenya, Tanzania, Zambia na nchi nyengine za dunia, pia huingia katika kundi hili la majina.Majina ya pekee pia hutaja Mito na maziwa, kama vile MtoTana, Rufiji kwa upande wa mito na Victoria, Tanganyika na mengineyo kwa upande wa Maziwa. Majina ya Milima kama, Elgon, Kilimanjaro nayo pia yamo katika kundi hili. Majina ya Bahari kana vile Hindi, Atlantiki na nyenginezo zimo kwenye kundi hili.

Majina ya mahali kwa uainishaji uliotajwa hapo juu ni sehemu ya majina ya pekee. Na hii ndio aina ya majina anayoshuhulikia mtafiti wakazi hii. Ukichunguza kwa makini utagundua kwamba majina hayo yamebeba maana inayotokana na utamaduni na mazingira ya jamii husika. Majina ya mahali hubeba maana na historia mbalimbali ambazo kimsingi hueleweka kwa wanajamii watumiaji wa lugha wenyewe kutokana na kuwa na maarifa elimu na uzoefu wa maisha. Pia majina haya, inawezekana hutolewa kutokana na matukio, historia, utamaduni ama athari mbalimbali zinazotokana na jamii. Maelezo ya wataalamu yanayohusu majina na aina zake yana mchango mkubwa kwa mtafiti, kwani atakapokutana na jina la mahali ataweza kubainisha jina hilo linatokana na kundi lipi miongoni mwa makundi ya aina za majina.

2.5 Kazi Tangulizi zinazohusu Majina ya Mahali

Cameroon (1961) anaeleza utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Waingereza. Ametoaaina mbili za majina ya mahali ambayo ni yale ya makazi na yale ya sura ya nchi ya eneo hilo. Mfano, Greenhill ikimaanisha eneo lenye kilima chenye rangi nyingi ya kijani.Kazi ya Cameroon (keshatajwa) inampa mtafiti kujua maeneo yapi yamefanyiwa utafiti kuhusu mada yake,na inamsaidia kugundua majina ya mahali yaliyotafitiwazamani na katika jamii tofauti.Kazi hii inatofautika na ya Cameroon kwa vile imejikita zaidi kwenye uchunguzi wamajina yamahali katikajamii ya kisiwa cha Pemba. Hymen (1964) anaeleza kuwa majina ya mahali yanaakisi fikra, watu pamoja navipengele vya utamaduni.

Chum (1982) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana Mkoa Kusini Unguja. Anataja majina kama vile Paje ambayo asili yake ni mnyama aitwae paa, pamoja na kilimo

cha chooko. Anasimulia kwamba, miongonimwa wageni waliofika Unguja walikuwa ni ndugu saba ambao walishauriana kuishi pembezoni mwa pwani ya Ungujaili waendeleze kilimo cha chooko Wakati wakijadiliana mmoja aliuliza tukiwa na kilimo hiki paa jee? Kwa vile paa wanapenda chooko. Kazi hii inampa dira mtafiti ya kugundua tafiti zilizofanywa na kuweza kufahamu asili za vijiji. Mlacha (1995) anaeleza asili ya majina ya mitaa inavyopatikana kisiwani Pemba. “Uvuani”asili yake ni kwamba, mahala hapa walihamia wageni wakawa wanafanyashughuli za uvuvi, wakaja watu wakawaulizauvuani, yaani unavua nini? Hapo ndipo kijiji hichokikaitwa Uvuani.

Zubeir (2015), anasema kwamba, “Micheweni”walikuwepo watu makatili wenye tabia ya kuwaua watu kutokana na imani ya kichawi. Hivyo watu walioishi mbali na eneo hilo walipaita Michawini linatokana na Uchawini lenye maana ya kuuwa, baadae pakaitwa Micheweni. Kazi hii itamsaidia mtafiti kupata ushahidi wa asili ya majina mbali mbali ya Mahali. Muzale (1998) anasema kuwa ingawa utoaji wa majina ni tukio la asili kwa jamii zote lakini kuna tofauti katika ubainishaji wa majina hayo, maana za majina hayo nazo hutofautiana toka jamii moja na nyengine.Hivyo, matukio yanayohusika kutoa majina ya mahali toka jamii moja na nyengine hayawezi kufanana kwani kila jamii ina taratibu zake. Utafiti wa Muzale (keshatajwa) utamuongoza mtafiti kugundua kuwa upo utofauti wa kazi yake na zilizotangulia kwani wamechunguza vigezo vya utoaji majina na maana za majina, wakati kazi hii inahusu uchunguzi wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahala kisiwani Pemba. Abuubakar (1998) ameeleza kuwa mtaa wa mtoni umepewa jina hilo kutokana na jengo kongwe la Sultani wa Zanzibar lililokuwepo

pembezoni mwa mto mdogo uliotokea upande wa ndani wa kisiwa cha Unguja, uliopitisha maji yake masafa mafupi kutoka kwenye jumba hilo kuelekea pwani.Abuubakar (keshatajwa), pia alieleza jina la Chuini, ambapo alisema kwamba jina hili asili yake kulikuwa na jumba kubwa lenye bustani kubwa ambapo walikuwa wakifugwa wanyama kama chui, simba na wengineo.

Scotsman (2003) anaeleza historia ya maana ya majina ya mahali katika jiji la Dar es Salaam. Alitumia majina ya vituo vya daladala na majina ya mitaa/kata. Alieleza majina ya vituo vya mabasi yanayotokana na majengo kama shule, hospitali, makanisa, watu maarufu, shughuli zinazofanywa na watu katika eneo hilo na uelekeo kituo kilipo. Alitoa mfano wa jina laNjia panda kwa Kawawa akasema kwamba kituo hiki kipo kwenye makutano ya njia inayoelekea kwa Kawawa.Pia anaeleza majina ya mitaa yanatokana mimea iliopo katika sehemu hiyo, lugha za asili, mfano, “Mwananyamala” yaani “mtoto usilie” ni neno la Kizaramo lililotolewa na wanawake walioishi awali katika eneo hilo kutumia usemi huu wakati wakibembeleza watoto wakiwa katika shughuli za shambani. Mengine hutokana na maeneo ambayo yanashabihiana, mfano, Mawenzi ya Dar es salaam ni eneo la mteremko kama ule wa“Mawenzi” ya Kilimanjaro.Buberwa (2010) alichunguza majina katika jamii ya wahaya akijikita katika majina ya mahali. Nae anakubaliana na Scotsman (kashatajwa)kwa kiasi kikubwa kwamba majina hutolewa kwa shughuli wanazofanya watu sababu za kihistoria, matukio, miti, mimea, wanyama, tabia, utamaduni na majanga ya asili mfano:Bwero ni jina la mahali palipotumika kunyongea wahalifu.

Ingram (2007) ameeleza asili ya neno Zanzibar ni “Zinjiba”linalotokana na lugha ya Kifursi, lenye maana ya ardhi nzuri ya watu weusi. Ingram (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba, neno Unguja lina asili ya Kiswahili linalotokana na neno” Ungujaa lenye maana ya kisiwa chenye watu wengi, vyakula tele na ibada nyingi.Ingram (keshatajwa) ameendelea kutoa maoni kwamba asili ya jina la Pemba, linatokana na neno la Kiswahili “kupemba” lenye maana ya kupembua ama kuongoza chombo kwa uangalifu kutokana na kisiwa hiki kuwa kimezungukwa na mkondo mkubwa wa bahari. Kazi hii nayo ni muhimu kwa utafiti huu kwani imetoa muelekeo wa kugundua baadhi ya majina ya mahala na historia zake.

BAKIZA (2011), wametaja majina ya mitaa inayopatikana mjini Unguja, sehemu alizokuwa akiishi mwanasanaa wajadi mashuhuri Bwana MSA. Wametaja jina la Kundemba, palikuwa maarufu kwa pombe za kienyeji na ngoma ya mbwakachoka (beni) pamoja na sherehe za tafrija.Baraste kipande, ulikuwa mtaa wa kukutanisha tamaduni za majumba yang’ambu.Kwa hivyo maelezo ya wataalamu hao walijikita zaidi na kueleza asili za mitaa lakini hawakuzingatia mazingira ya kimaumbile yanavyoibua majina yamahala katika maeneo hayo.

Kipindi cha Redio Nour (2013), kimesimulia asili ya mitaa inayopatikana kisiwani Pemba. Kijiji cha Tasini, kilipewa jina hilo kwa sababu lilikuwepo eneo dogo lenye kukaa maji. Wema na waje, ni mtaa uliokuwa ukikaliwa na Waarabu weusi, waliojitenga na watu, wakiishi peke yao, wakawa wanasema, sisi tuko huku wema na waje. Asili ya Kiuyu inasemekana kuwa alikuwepo bibi Bi.Kirembwe ambaye alikuwa ana tabia ya ushirikina, watu walikuwa hawampendi na alitengwa na watu. Aliamua kuhama, lakini alipata tabu alikokwenda, hivyo aliamua kurudi tena

kijijini.Watu walipomuona walisema kile kibibi, Kiuyu, yaani kimerejea. Maelezo hayo yalisimulia tu asili za vijiji hayakujihusisha na uchunguzi wa mazingira ya kimaumbile jinsi yanavyochangia kuibua majina ya mahala kisiwani Pemba.

Kwa mantiki hiyo majina kwa ujumla ni matokeo ya wanajamii kulingana na maisha yao na jinsi wanavyofanya kazi.Kwa ujumla kazi tangulizi zilizopitiwa zimetoa mchango mkubwa kwa kufanikisha kazi hii ingawa kazi nyingi zilijikita kueleza asili, maana na matumizi ya majina ya mahali katika jamii mbalimbali za Kibantu na Afrika kwa ujumla lakini hazikueleza mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba.

2.6 Mkabala wa Kinadharia

Sengo (2009) anasema nadharia niwazo kuu,mwongozo wa mtu au watu, wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani.Kombo naTromp (2006) wanasema kiunzi cha nadharia ni mkusanyiko wa mawazo yatumikayo kuelezea jambo fulani. Ni mawazo yatokanayo na mantiki yenye kuafikiana na utambulisho wa kidata.Ili kufikia malengo ya utafiti huu tutatumia nadharia jumuishi ya Giles (1979). Kwa jamii ya Wapemba kuendelea kutumia majina ya mahali ni ishara ya kuthamini tamaduni zao historia na lugha pamoja na umoja wao wa kiudugu.Hivyo nadharia hii inatumika katika utafiti huu kwa sababu imehusisha vibainishi jumuishi kadhaa ambavyo vimetumika kwa pamoja kubainisha majina ya mahali katika jamii yaWapemba.Nadharia hii inahusisha vibainishi vingi vya kijamii ambavyo humtambulisha mzungumzaji. Msingi wa nadharia hii unazingatia fasili ya jamii lugha inayosema kuwa jamii lugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamii lugha moja ambayo ikotofauti

na jamii lugha nyengine (Msanjila na wenzake, 2011). Kutokana Giles, asili ya mtu ndio inayotoa utambulisho wa mtu. Nadharia hii inayoongoza utafiti huu katika kubaini mazingira ya kimaumbile yanavyochangia kuibua majina ya mahala katika kisiwa cha Pemba.

2.7 Hitimisho

Katika sura hii vipengele kadhaa vimejadiliwa. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na kazi tangulizi ambazo zinahusiana na mada husika pamoja na mkabala wa kinadharia utakao tumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea utaratibu na mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Vile vile sura hii imeelezea mbinu zitakazotumika kuchanganua data zilizokusanywa na kujadiliwa katika utafiti huu. Opie (2010) anaeleza kuwa mbinu za utafiti ni michakato au hatua za kitaaluma za kupata taarifa kwa kuzingatia njia ambazo zilipelekea kupata data za uhakika kuhusiana na utafiti unaofanyika.

3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika mkoa kusini na mkoa wa kaskazini ya kisiwa cha Pemba. Sehemu zitakazotumika ni wilaya ya Mkoani, wilaya ya Chakechake, wilaya ya Wete, pamoja na wilaya ya micheweni. Data zilikusanywa kwa njia ya udodosaji na mahojiano na uchanganuzi wa data utafanywa kwa njia ya kimaelezo kwa sababu ni “muundo unaoweza kutumika kwa tafiti ambazo zina lengo la kujua tabia,mielekekeo na mawazo ya watu” Orodho na Kombo (2003). Hivyo basi mtafiti ameteuwa muundo huu kwa vile utafiti wake unahusiana na uchunguzi wa mazingira ya kimaumbile yanavyoweza kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo mtafiti atahitaji maelezo kujua historia za mazingira ya kimaumbile kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba. Kwa hakika data zilichanganuliwa kulingana na madhumuni ya utafiti yaliyowekwa. Njia ya takwimu haikutumika ila pale ilipolazimika na hata hivyo takwimu zilipotumika pia zilichambuliwa kwa maelezo.

3.3 Kundi Lengwa

Babbie (1999) anafafanua kundi lengwa kuwa ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika populesheni kuu ambalo hutoa data za kuwakilisha kundi kubwa. Nae Cooper (1989) amefasili kundi lengwa kama ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Hivyo kundi lengwa ni sehemu kutoka katika kundi kubwa ambayo huwakilisha kundi lote.

Katika utafiti huu kundi lengwa mahususi ni kama ilivyoelezwa katika jadweli no.3.1, ambapo wazee wa vijiji 40 kwa wilaya zote nne, ambazo ni wilaya ya chake chake,wilaya ya mkoani, Wilaya Wete pamoja na wilaya ya Micheweni. Wanajamii wengine watakaotumika kwa wilaya ya chakechake ni 12, Wilaya mkoani 8, wilaya ya wete 15 na wilaya ya Micheweni ni 6. Kutokana na mchanganuo huo tunapata jumla 81.

3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu utafanyika katika maeneo mbalimbali yakisiwa cha Pemba ikihusisha mikoa miwili ambayo ni Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini. Mkoa wa Kusini una jumlaya wilaya mbili ambazo ni wilaya ya Mkoani na wilaya ya Chake chake. Mkoa wa Kaskazini una wilaya yaWete na wilaya ya Micheweni. Baadhi ya majina yanayopatikana katika maeneo mbalimbali ya wilaya zilizotajwa hapo juu ndiyo yaliyohusishwa katika ukusanyaji wa data za uwandani. Upendeleo katika uteuzi wamaeneo ulihusu maeneo yote yenye kuhusiana namada husika. Kwa upande wa wilaya ya Mkoani, utafiti ulifanyika katika maeneo mbalimbali kama vile Kidutani, Changaweni na mengi mengineyo. Wilaya ya Chakechake maeneo yaliyofanyiwa

utafiti ni Chanjamjawiri, Ndagoni, Uwandani, Mchangani pamoja na Dumbini. Kwa upande wa wilaya ya Wete utafiti huu ulifanyika katika maeneo kama vile Mtemani, Kilima Ndege n.k. Kwa upande wa wilaya ya Micheweni utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Vilima Vitatu, Mawe Matatu n.k. Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kutokana na upatikanaji wa maeneo ambayo yameitwa majina kutokana na mazingira ya kimaumbile. Sababu nyingine ya kuchagua maeneo ya kisiwa cha Pemba ni kwamba katika kupitia kazi tangulizi mbalimbali mtafiti hakugundua maandishi yanayoeleza kuhusu mazingira ya kimaumbile yanavyochangia kuibua majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Kwa mujibu wa Babbie (1999) na Kothari (2008) wamefafanua kuwa, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linaloteuliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo data za kuwakilisha kundi kubwa hupatikana. Kutokana na ukweli kwamba sio jambo jepesi kwa mtafiti kuwatafiti watafitiwa wote ndio maana kunateuliwa sampuli ya utafiti.

Usampulishaji kwa mujibu wa sigh (2007) ni ule mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kwa kuwa ni vigumu kuwatafiti watu wote wanaoishi katika eneo la utafiti. Mtafiti alichaguwa sampuli ambayo ndio hasa iliyotumika kuwakilisha wengine. Kwa upande wa uteuzi wa sampuli ya maeneo na watafitiwa, Mtafiti alijikita na kuangalia zaidi katika uwepo wa data zinazohitajika kwa kuangalia mada na malengo ya utafiti huu. Maeneo yalioteuliwa ni zile sehemu zenye mazingira ya kimaumbile na ambayo yalipelekea upatikanaji wa taarifa muhimu za utafiti huu. Sehemu ambazo zinapatikana katika wilaya nne za Pemba, Mtafiti alikusudia kuteuwa vijijini arobaini

ambapo kila wilaya aliteuwa vijiji kumi kwa kutumia mbinu bahatishi ama kwa upande wa kuwapata watafitiwa, Mtafiti alitumia mbinu ya Kothari (2008) Mbinu ya kukusudia na mbinu ya kubahatisha (bahati nasibu) ili kupata taarifa zinazohitajika katika utafiti huu, mtafiti anakusudia kuteuwa makundi mawili ya watafitiwa ambayo ndio hasa alitarajia kupata data zilizowiana na mada pamoja na malengo ya utafiti huu. Kundi la kwanza linalowahusisha wazee ambao wanahusika katika Mazingira/maeneo ambayo yalitafitiwa wakiwa jumla 40 ambapo kila wilaya wazee 10. Kundi la pili lilihusisha wanajamii wengine ambapo katika wilaya ya Chakechake ni 12, mkoani 8, Wete 15 na Micheweni 6 Jumla ni 41. Hivyo idadi ya watafitiwa wa utafiti huu inaoneshwa kwa muhtasari katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.3.1: Makundiya Watafitiwa, Maeneo watokayo na Idadi yao

Na.		Wazee wa Vijiji husika	Wanajamii wengine	Jumla
	Wilaya ya Chake Chake	10	12	22
	Wilaya ya Mkoani	10	8	18
	Wilaya ya Wete	10	15	25
	Wilaya ya Micheweni	10	6	16
Jumla		40	41	81

Chanzo: Data kotuka Uwandani

Jedwali hili linaonesha usawa katika uteuzi wa wazee wa vijiji lakini linaonesha tafauti kubwa katika upande wa wanajamii wengine. Sababu kubwa alioizingatia

mtafiti ni ukubwa wa eneo husika pamoja na wingi wa wakaazi wa maeneo hayo, sambamba na upatikanaji wa mzingira / maeneo anavyotarajia kufanyia utafiti.

3.4.2 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (1990) anasema mbinu ya kukusanya data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Best na Kahn (1993) wakisisitiza umuhimu wa kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data wanasema kuwa, kila mbinu ya kukusanya data ina ubora na changamoto zake. Njia moja wapo ya kupunguza changamoto na kuongeza ubora ni kutumia mbinu zaidi ya moja katika utafiti. Hivyo, katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu za hojaji na mahojiano. Mbinu hizi zilitumika sambamba na upitiaji wa nyaraka na kumbukumbu muhimu ili ziweze kukamilishana.

3.4.3 Hojaji

Hojaji au udodosaji nimbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti huandaa maswali yanayoelekeza namna ya kujibu na kuwapa watafitiwa ili wayajibu (Enon1998). Kwa upande mwengine Kothari (1990) anasema kwamba, hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yameshajibiwa. Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, ambayo ilimsaidia sana katika kufanya ulinganifu wa majibu yaliyopatikana kwa watafitiwa wote. Mtafiti anaamini kuwa hojaji ni njia rahisi kupata taarifa kwa watafitiwa wengi kwa wakati mmoja. Vilevile, njia hii ni rahisi na husaidia kuokoa muda, lakini pia husaidia kutunza siri. Mbinu hii ilitumika kukusanya data kutoka kwa viongozi wa serikali katika maeneo husika.

3.4.4 Mahojiano

Kwa mujibu wa Enon (1998) mahojiano ni mbinu ya kukusanyia taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya ana kwa ana. Mbinu hii humuwezesha mtafiti kuhoji watu binafsi au kundi maalum kwa maswali madogo madogo yanayohusu suala lake la utafiti. Mahojiano hayo yalifanywa kwa hali ya nusufunge, baadhi ya maswali kutayarishwa kabla ya mahojiano na mengine kutolewa na mtafiti papo kwa papo. Mbinu hii ilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka kwa wanajamii walioko kwenye vijiji vilivyoteuliwa. Mbinu hii ni nzuri kwani humsaidia mtafiti kupata taarifa za ziada zitakazotolewa na watafitiwa baada ya kuwauliza maswali ya ziada jambo ambalo sio rahisi kupatikana katika mbinu ya hojaji. Pia ilimsaidia mtafiti kupata mawazo na mitazamo ya watafitiwa kuhusu anachokichunguza.

3.5 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Steere (2010), mkabala wa maadili ni moja miongoni mwa masuali muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito mkubwa wakati akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Adam na Kamuzora (2008) wametaja maadili ya utafiti kuwa ni haki ya kuwa nasiri, yaani mtafiti kutotoa siri za mtafitiwa.Pia mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, hakiya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu suali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.Mtafiti anatambua haki zote hizi na anaahidi kuzifanyia kazi. Utafiti huu ulizingatia misingi yote ya utafiti ikiwa ni pamoja nakupata ridhaa ya wahojiwa, uhuru wa kushiriki kwa watafitiwa wote watakaopata fursa ya kuchaguliwa kushiriki katika utafiti huu. Kila mtafitiwa ali pewa taarifa kamilikuhusu mada ya utafiti ili kuweza kuchangia kwa uwazi zaidi

katika kutoa data. Mtafiti alihakikisha kwamba anakwenda sambamba na maadili ya kitaaluma wakati wote wa kutekeleza utafiti wake na kuficha siri za watafitiwa.

3.6 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa kiasi kikubwa mbinu zitakazotumika katika utafiti huu, mpango wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, pamoja na maadili ya utafiti. Kwa jumla, mbinu zote hizi kwa pamoja ndizo ambazo zimetumika katika kukusanya na na kuchambua data za utafiti huu na kuuwezesha kukamilika.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili data kuhusu malengo makuu ya utafiti ambayo yanachunguza mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali kisiwani Pemba. Sura hii ina shabaha ya kuyachambua malengo ya utafiti huu ambayo ni Kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile yanayochangia upatikanaji wa majina ya mahali kisiwani Pemba na Kuchunguza historia ya mazingira ya kimaumbile kuibuka kwa majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba. Katika lengo la kwanza vijiji mbalimbali ambavyo vimeibuka kutokana na mazingira ya kimaumbile vimejadiliwa maeneo yao ya kijiografia na mipaka pamoja na mipaka yao. Katika lengo la pili, mtafiti alijibu swali namba mbili la utafiti linalohusuhistoria ya mazingira ya kimaumbile jinsi yalivyojitokeza katika kuibua kwa majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba. Katika lengo hili historia na asili ya vijiji vingi zilitajwa na kubainishwa kwa uwazi na kuangazia jinsi nadharia teule ilivyoakisi uchambuzi ulioainishwa.

4.2 Majina ya Mahali yaliyoibuka kutokana na Mazingira ya Kimaumbile

Lengo la kwanza la utafiti huu kama ilivyobainishwa kwenye (1.4.2) ni kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile kisiwani Pemba. Katika sehemu hii majina yasiyopungua (41) yamebainishwa na kufafanuliwa kwa ufupi maeneo yake ya kijiografia. Mipaka ya kila eneo imebainishwa na kuwekwa wazi. Ufafanuzi wa maeneo/mahali humo umewekwa wazi kama ilivyo kwenye 4.2.1-2.2.41 hapo chini:-

4.2.1 Kijiji cha Mivumo Ishirini

Mivumo ishirini ni kijiji kidogo kilichoko ndani ya Jimbo la Ziwani, wilaya ya Chakechake Pemba. Kijiji hiki kimo ndani ya shehia ya Ziwani. Kwa upande wa mipaka yake, mtafiti alihudhuria huko na kutembezwa na mwenyeji wake bi Fatma Rashidi Mohad. Matembezi hayo yalifanyika siku ya tarehe 27/05/2018 huko Ziwani, Mivumo ishirini. Kusini ya kijiji cha Mivumo ishirini mtafiti alibaini kuna kijiji kiitwacho Kifugwe Mbuzini, kaskazini kuna eneo ljulikanalo kwa jina la kwa Mwanamwari, Magharibi ya Mivumo ishirini kuna kijiji cha Mwavungwa na mashariki kuna kijiji kiitwacho Mbuzini Chanjaani. Kama walivyo wakaazi wengi wa Pemba watu wa mivumo Ishirini wengi wao ni wakulima na wengine ni wajasiri amali wa shughuli mbalimbali. Idadi ya watu wanaoishi ndani ya kijiji cha Mivumuo Ishirini si kubwa. Kiasi cha kaya sitini hadi sabiini za watu zinaishi huko. Wakaazi wa Mivumo ishirini wengi wao ni wakulima wa kilimo cha kujitafutia mazao ya kujikimu.

4.2.2 Kijiji cha Kidutani (Kidutani cha Bamkuja)

Kidutani ni kijiji kilichoko wilaya ya Mkoani, Mkoa wa kusini Pemba. Kijiji hiki kimo ndani ya jimbo la Mtambile, shehia ya minazini. Kijiografia Kidutani iko kusini mashariki ya kisiwa cha Pemba. Kidutani iko katikati na imepakana na kijiji cha Mkungu kwa upande wa kusini. Kaskazini imepakana na kijiji cha Mabieni. Mashariki imepakana na kijiji cha Nanguji, na upande wa magharibi imepakana na kijiji cha Mitatuni. Kwa kukisia kijiji cha Kidutani kina ukubwa wa kilomita za mraba zisizopungua thelathimi (30). Idadi ya watu wanaioshi kwenye kijiji hiki ni zaid ya mia moja na tisiini. Wakaazi wa kijiji hiki wengi wao wanafanya kazi za

kilimo. Zaidi wanajishughulisha na kilimo cha kuhuwisha mikarafuu na vipando vya muda mfupi kama vile mihogo, mpunga, viazi vidogo na vipando vyengine kutegemeana na misimu ya mvua.

4.2.3 Kijiji cha Bubujiko

Bubujiko ni miongoni mwa vijiji vinavyopatikana katika mkoa wa kaskazini Pemba, wilaya Wete, shehia ya Jadida kwenye jimbo la Wete. Upande wake wa kusini kijiji cha Bubujiko kimepakana na kijiji cha Uchozini, Kaskazini kuna mtaa wa Mtemani, Mashariki ya Bubujikokuna kijiji cha Jadida na kwa upande wake wa Magharibi Bubujiko iko jiranina kijiji cha Kipangani na Uzunguni. Bubujiko ni mtaa miongoni mwa mitaa iliyoko Wete. Kwa kuwa huu ni mtaa ulioko mjini bila shaka idadi ya watu wake si ndogo sana. Kaya zaidi ya mia mbili zinapatikana katika kijiji cha Bubujiko. Wakaazi wa Bubujiko ni watu wa mjini kwa hivyo shughuli zao ni mchanganyiko kama walivyo watu wa mij mingine. Wengine huvua, wengine hujishughulisha na kilimo na baadhi yao ni wafanya biashara.

4.2.4 Kijiji cha Mtoni Msengele

Mtoni Msengele ni kijiji kinachopatikana katika Mkoa wa kusini Pemba. Kijiji hiki kiko katika wilaya ya mkoani. Kijiji hiki kinapatikana katika shehia ya kiwani ambayo imo ndani ya jimbo la Kiwani. Kijiji hiki kimepakana na kijiji cha Kumbi kwa upande wa mashariki. Upande wa kusini Mtoni Msengele imepakana na vijiji viwili ambavyo ni Mikinduni na Kivumoni. Kaskazini mwa Mtoni Msengele kuna kijiji cha Msengele, ilhali upande wake wa magharibi kuna kijiji cha Mtadoda. Idadi ya wakaazi wa Mtoni Msengele ni zaidi ya mia moja na ishirini (120). Watu wa Mtoni Msengele zaidi hujishughulisha na kilimo, hasa vilimo vya msimu,

kutegemeana na misimu ya mvua. Kilimo cha mananasi ni mashuhuri zaidi kijijini hapo.

4.2.5 Kijiji cha Jiweni

Jiweni ni kijiji kilichopo mkoa wa kaskazini Pemba, wilaya ya Micheweni, shehia ya Tondooni, jimbo la Konde. Kwa upande wa kusini Jiweni imepakana na bahari ya Hindi. Upande wa kaskazini Jiweni imepakana na kijiji cha Mkia wa ng'ombe. Mashariki kjiji cha Jiweni kimepakana na msitu wa hifadhi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uitwao Msitu wa Ngezi. Magharibi Jiweni imepakana na kijiji kiitwacho Bandari Kuu. Wakaazi wa Jiweni hujishughulisha zaidi na shughuli za kilimo na uvuvi. Idadi ya wakaazi wake ni ndogo sana. Watu wanaoishi hapo kwa jumla hawazidi mia moja. Wakaazi walio wengi wa eneo hili ni wavuvi na baadhi yao ni wakulima wa mwani huko pwani na mazao ya muda mfupi yanayotegemea mvua za misimu. Viazi vitamu na muhogo ni kilimo kilchoshika kasi zaidi kwenye eneo hili.

4.2.6 Kijiji chaNdaambani

Ndaambani ni eneo linalopatikana kwenye mkoa wa kaskazini Pemba, kwenye wilaya ya Micheweni. Nadaambani iko ndani ya eneo la shehia ya Tondooni na limepakana na kijiji cha Mkia wa Ng'ombe kwa upande wa kusini. Kwa upande wa kaskazini Ndaambani imepakana na eneo la Shanzu. Mashariki ya Ndaambani kunapatikana msitu mkubwa wa hifadhi ya serikali uitwao Msitu wa Ngezi. Upande wa magharibi ya Ndaambani kuna bahari ya Hindi. Ndaambani ni kijiji kidogo sana chenye wakaazi wachache mno. Wakaazi wengi wa jinsia ya kike kijiji hiki ni wakulima wa mwani, ilhali wale wakiume ni wavuvi wa kawaida. Wavuvi wa eneo

hili san asana huwenda kwenye kambi za ago nje ya Pemba. Wapo waendao Tanga na wengine sehemu za Mombasa huko Kenya.

4.2.7 Kijiji cha Mchangani

Ni moja kati ya eneo linalopatikana kaskazini Pemba. Wilaya ya micheweni, shehiya ya Tondoni, jimbo la konde. Mchangani ni sehemu ya ago ambayo hukaliwa na wavuvi kutoka katika kijiji cha mkia wa ng`ombe. Upande wake wa kusini imepakana na bahari, kwa upande kaskazini imepakana na msitu wa ngezi, mashariki pia imepakana na bahari. Kiufupi eneo hili sehemu zake zote zimepakana na bahari isipokuwa upande wa kaskazini ndio ambayo imepakana na msitu wa ngezi. Ni sehemu inayotumiwa kwa makaazi ya wavuvi wa ago.

4.2.8 Kijiji cha Miti Ulaya

Miti ulaya ni mmoja kati ya mitaa iliyopo katikati ya mji wa Wete ambapo katika utawala wa Wareno ndipo ilipopitishwa barabara kuu iliyounganisha mtaa huu na mitaa mingine ya mji wa Wete. Miti ulaya ni mtaa wa bandari na kwa hivyo umepakana na bahari ya Hindi kwa upande wa Magharibi, upande wa Mashariki umepakana na mtaa uitwao Selemu ulio katikati ya mji wa Wete. Kusini ya Miti Ulaya kuna eneo liitwalo Machinjioni na Kaskazini kuna mtaa uitwao Majimbikani. Miti Ulaya inaonekana ndiyo kitovu cha mji wa Wete kwa kuwepo kwa bandari, soko kuu la Wete na moja miongoni mwa shule kubwa za mji wa Wete. Shule hiyo inaitwa kwa jina hilo la Shule ya Miti Ulaya. Shule nyengine za sekondari zilizoko Wete ni Utaani, Chasasa, Limbani na Kizimbani. Pia ipo shule iitwayo Wete Sekondari. Wakaazi wa Miti Ulaya sio wengi sana kwa kuwa zaidi eneo hili ni la

biashara na shughuli za kijamii na sio eneo maalum kwa makaazi ya binaadamu. Familia nyingi ziishizo hapo ni za wafanya kazi wa serikali.

4.2.9 Kijiji cha Mawe Matatu

Mawe matatu ni kijiji kilichopo katika shehia ya Makangale, jimbo la Konde, mkoa wa kaskazini Pemba. Kijiji cha Mawe matatu kipepata bahati ya kupakana na bahari ya Hindi kwenye pande zake mbili; kaskazini kwa upande mmoja na magharibi kwa upande wa pili. Kusini ya kijiji cha Mawe matatu kuna kijiji kikubwa cha Makangale. Mashariki ya Kijiji cha Mawe matatu kuna eneo la hoteli za kitalii liitwalo Vuma Wimbi. Eneo hili ni la rasi iliyojitokeza zaidi katika kisiwa cha Pemba. Shughuli kubwa zinzofanywa na watu wa Mawe Matatu ni kilimo na uvuvi. Mawe matatu ni kijiji kidogo sana kiasi ambacho wakaazi wake hawazidi hamsini kwa kuchanganya na watoto chini ya umri wa kwenda shule.

4.2.10 Kijiji cha Chanjamjawiri

Chanjamjawiri ni mtaa unaopatikana katika shehia ya Shungi, wilaya ya Chake chake, mkoa wa Kusini Pemba. Kimipaka Chanjamjawiri imepakana na Matale kwa upande wa kusini, kaskazini imepakana na Limani, mashariki imepakana na Pujini na Chanjaani na kwa upande wa magharibi imepakana na Shungi. Wazee wawili; bwana Salim Seif Salim na Salim Mata walipokuwa wanahojiana na mtafiti wa kazi hii walisema mtaa huu hapo mwanzo ulijulikana kwa jina la Kilimani na kwa sasa unajulikana kwa jina la Chanjamjawiri. Chanjamjawiri ipo kilomita Tisa nje ya mji wa Chakechake. Wakaazi wake wengi ni wakulima na wamilki wa mashamba makubwa ya mikarafuu. Wapemba wengi wenye asili ya Kiarabu waliishi na

kujifanyia makaazi katika eneo hilo. Chanjamjawiri mbali ya kwamba si eneo kubwa ila wakaazi wake ni wengi si haba.

4.2.11 Kijiji cha Kilimandege

Kilima ndege ni kilima amabacho kipo katikati ya mji wa Wete. Kijiji hiki kipo kwenye njia kuu kutoka bandarini kuelekea kwenda sehemu mbali mbali za kisiwa cha Pemba. Kilimandege ni mtaa uliopakana na mtaa wa Sebuwatu kwa upande wa Kaskazini, Kusini yake kuna Kipangani juu, Magharibi kuna Selemu na Mashariki kuna Mtemani. Kwa ufupi mtaa huu umeitwa Kilimandege kwa kuwa, ni sehemu iliyojuu ya kilima na iliyokuwa mapumziko ya ndege kabla miti mikubwa haijakatwa na mazingira ya eneo hilo kugeuzwa makazi ya watu. Ni katika eneo la Kilimandege ambapo Makao Makuu ya Polisi ya mkoa wa kaskazi Pemba yanapatikana. Ni sehemu ndogo mno kieneo na kwa hivyo wakaazi wake pia sio wengi. Wakaazi wake ni wafanya biashara na watumishi wa umma kwa kuwa nyumba za wafanya kazi wa serikali wanapatikana hapo.

4.2.12 Kijiji cha Minazini

Minazini ni kijiji kilichopo pembezoni mwa mji wa Chake, kaskazini magharibi ya mji huu na kwa kweli tunaweza kusema kijiji hilki kimepakana na mji wa Chake chake**.** Kijiji hiki kikobondeni na kimepakana na kijiji cha Ngomahazingwa kwa upande wa kaskazini hasa kwenye pembe yake ya magharibi. Mipaka yake kwa upande wa kusini ni kijiji cha Tibrinzi, ilhali mashariki kuna Chachani kwa upande mmoja na Mkungumalofa kwa upande wa kusini mashariki. Upande wa magharibi kuna Pondeani. Kijiji hiki kinaonekana bondeni pembeni mwa bara bara inayoelekea

Wete. Minazini ni kijiji chenye kaya zisizopungua mia moja na ishiri. Wakaazi wake wengi ni wafanya kazi wa kujitegemea (wajasiri amali).

4.2.13 Kijiji cha Tibirinzi/Kibirnzi

Tibirinzi ni kijiji kilichopo kaskazini Magharibi ya mji wa Chake. Tibirnzi au kwa jina jengine Tibinzi iko juu ya kilima kuuelekea ukanda wa pwani iliyojitokeza kama eneo la rasi karibu na soko jipya liitwalo kwa jina la Katar. Sehemu nyengine ya Tibirinzi iko bondeni kuelekea eneo la hifadhi ya mikoko na kuelekea ikulu ndogo ya Chakechake. Upande wa magharibi Tibirinzi imepakana na kijiji cha Pondeani. Mashariki ya Tibirinzi kuna kijiji cha Chachani, ilhali kusini yake kuna mtaa wa Misufini. Kaskazini ya Tibirinzi kuna mtaa wa Minazini. Ni katika mtaa wa Tibirinzi ambapo uwanja mashuhuri wa mikutano ya kisiasa na shughuli za serikali hufanyika. Ni eneo ambalo wakiristo wamejikita kwa kiasi. Kanisa kubwa la Kikatoliki na kanisa jengine la Kiangilikana linapatikana huko. Nusu ya eneo la Tibirinzi ni muinuko mkubwa na nusu nyengine ni bonde lililoteremka kuelekea ikulu ndogo Chake chake Pemba. Wakaazi wachache wa Tibirinzi hujishughulisha na biashara.

4.2.14 Kijiji cha Mtoni Chakechake

Mtoni miongoni mwa vijiji vikongwe vinavyounda mji wa Chakechake. Kijiji cha Mtoni kinapakana na eneo liitwalo Afrikana kwa upande wa kusini. Kusini mashariki ya Mtoni kuna Shamiani na Madungu. Kaskazini Mtoni imepakana na kijiji kidogo sana kiitwacho Lamu, Kaskazini magharibi kuna kijiji kiitwacho Mtambuuni, ilhali kaskazini mashariki Mtoni imepakana na Michakaini. Mtoni imepakana na Msingini kwa upande wa magharibi. Mtoni ni sehemu ya mjini na kwa hivyo watu wake wengi hujishughulisha na biashara za aina mbalimbali. Wengine bilashaka ni wakulima

wanaoendesha shughuli zao za kilimo nje ya mji wa Chakechake. Wakaazi wa Msingini ni wengi sana kwa sababu ni enep lililoshiba na kusheheni nyumba za makaazi ya raia. Idadi ya watu kwa kukisia ni zaidi ya mia sita ukihusisha na watoto wadogo.

4.2.15 Kijiji cha Mbuyu Mkavu

Kiukweli eneo la Mbuyu Mkavu si eneo la makaazi ya watu. Eneo hili ni eneo la utalii, lililojitenga upande wa mashariki ya kijiji cha Vitongoji. Kwa upande wake wa mashariki eneo la Mbuyu Mkavulimepakana na bahari ya Hindi. Limepakana na bahari kuu yenye mwamba mkali kabisa uvumao upande wa mashariki. "*Bwana Khatib Makame Haji aliehojiwa siku ya tarehe 22/05/2018 anasema katika bahari hiyo hakupiti chombo chochote cha kuvulia wala kusafiria zaidi ya mameli makubwa ya kimataifa. Watu wa Vitongoji huiita bahari hiyo kuwa ni bahari dume*". Magharibi ya eneo la Mbuyu Mkavu kuna maeneo ya kilimo ambayo hupandwa mazao mbali mbali na wakaazi wa Vitongoji. Mazao mashuhuri yalimwayo hapo ni karanga, mahindi, vyakula jamii ya vitango, mbaazi, nyanya, nyanya chungu na mabiringanya pamoja na mazao mengi menmgineo. Ni katika eneo hili ambapo machimbo ya mawe kwa ajili ya ujenzi hupatikana. Kiwanda cha kuvunjia kokoto pia kipo kwenye eneo hili. Kaskazini mwa Mbuyu Mkavu kuna msitu uliojaa tele miti pori mikubwa na midogo. Miongoni mwa miti pori ipatikanavyo hapo ni mikwamba, midimu msitu na miti mingi mingineo. Kusini ya eneo la Mbuyu Mkavu kuna gofu maalum, miongoni mwa magofu mengi ya kihistoria yanayopatikana mashariki ya kijiji cha Vitongoji. Gofu hili hujulikana kwa jina la gofu la Likoni.

4.2.16 Kijiji cha Mvumoni

Kijiji cha Mvumoni kipo eneo la karibu sana na uwanja wa ndege wa Karume ulioko Mfikiwa. Upande wa kaskazini Mvumoni imepakana na Furaha, Kusini ya kijiji cha Mvumoni kuna kijiji kiitwacho Mtimbu. Mashariki ya Mvumoni kuna bahari ya Hindi ya ukanda wa makaani, mashariki ya kisiwa cha Pemba. Upande wa magharibi ya Mvumoni kuna mfikiwa ambako uwanja wa ndege wa Pemba unapatikana. Kijiji cha Mvumoni ni kikubwa sihaba. Kina kaya zisizopungua mia mbili. Wakaazi wengi wa kijiji hiki ni wavuvi na wakulima. Kijiji hiki pamoja na vijiji vilivyojirani yakevinazalisha mazao mengi ya jamii ya vitango. Mazao hayo ni pamoja na maboga, vitango pepeta, matikiti maji, mamungunye na mazo mengine ya aina hii. Mazao mengine yanayolimwa hapo ni nyanya, mabilingani na nyanya chungu ambazo Wapemba huziita nyanya mshumaha. Karanga na kunde ni zao mashuhuri zaidi kati ya mazo yazalishwayo hapo.

4.2.17 Kijiji cha Mkungupigi

Mkungupigi ni kijiji kinachopatikana katika shehia ya vitongoji. Vitongoji iko upande wa mashariki yapata kilomita nne na nusu kotuku mji wa Chakechake. Mkungupigi ni kijiji kilichopakana na shule ya Vitongoji kwa upande wake wa mashariki. Kaskazini kijiji cha Mkungupigi kimepakana na kijiji jirani cha Udusini. Kusini yake kuna kijiji cha Vikutani, ilhali magharibi kuna nyumba za vijiji vya ujamaa kwenye kijiji kiitwacho Vijijini. Idadi ya wakaazi wa Mkungupigi sio kubwa, kutokana na udogo wa kijiji chenyewe. Wakaazi wake kutokana na taarifa aliyeitowa mtafitiwa Bishara Nassor aliyehojiwa mnamo mwishoni mwa April 2018 ni kama

sitini. Wakaazi wake wanajishughulisha zaidi na kilimo na wachache kati yao ni wavuvi.

4.2.18 Kijiji cha Mavani Chaka la Kati

Chaka la kati asili yake ni eneo lililokuwa na chaka kubwa kata itakavyoelezwa kuko mbele kwenye kipengele nambari 4.3.18. Kwa sasa Chaka la kati ni eneo linaloishi watu. Ni kijiji katika shehia ya Chambani, jimbo la chambani, wilaya ya mkoani, mkoa wa kusini Pemba. Kijiji hiki kimepakana na kijiji cha Makumbi kwa upande wa kusini. Kaskazini mwa kijiji cha Chaka la kati kuna kijiji cha Maambani. Mashariki kuna bahari ya Hindi, eneo liitwalo bahari ya Kikokwe. Magharibi ya Chaka la Kati kuna kijiji kiitwacho Shangini.

4.2.19 Kijiji cha Mikarafuu Giza

Mikarafuu Giza ni kijiji kilichopo wilaya Mkoani, mkoa wa kusini Pemba. Upande wake wa kaskazini Mashariki kuna kijiji kiitwacho Mkwajuni, ilhali kaskazini magharibi kuna ufimbi wa mto wa maji na magharibi hasa kuna mashine ya maji inayotumika kusukuma maji ya mto huu na kuyapeleka sehemu nyengine wanazoishi raia. Kusini ni sehemu isiyokaliwa na watu yenye kijipori kidogo kilichosheheni miti mingi aina ya mianzi. Kusini mashariki kuna eneo liitwalo kijogooni na mashariki wenyewe kuna sehemu ya mto wa maji vile vile. Hii ndiye mipaka ya Mikarafuu Giza.

4.2. 20 Kijiji cha Mavapacha

Kijiji cha Mavapacha kiko katika shehia ya Wawi, jimbo la Wawi, wilaya ya Chakechake, kisiwani Pemba. Eneo hili liko njiani kuelekea Magogoni kwendea

uwanja wa ndege kupitia njia za ndani. Mavapacha imepakana na kijiji kimoja kilichojengwa nyumba za maendeleo miaka ya mapema sabiini. Kijiji hiki chenye nyumba za maendeleo huitwa Vijijini. Hiki ni kijiji walichopakana nacho kwa upande wa magharibi. Upande wake wa kusini kuna kijiji kiitwacho Kichangani. Kaskazini kuna Kunguni, ilhali mashariki kuna kijiji kiitwacho Bigilini. Bigilini ipo karibu sana na kaburi la Dakta Omari Ali Juma, aliyekuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania kati ya mwaka 1995 hadi 2001. Hili ni eneo la mava linalotumika hadi leo kuzikwa watu.

4.2.21 Kijiji cha Mkoroshoni

Mkoroshoni ni kijiji kilichopo kilomita mbili na nusu kutoka mjini Chakechake. Kijiji hiki kipo baina ya kijiji cha Mkanjuni na Gombani. Hiki ni kimoja miongoni mwa vijiji vikubwa vinavyopatikana katika wilaya ya Chakechake. Ni kijiji chenye wakaazi wengi wasiopungua elfu moja na mia tano. Kaskazini mwa Mkoroshoni kunapatikana kijiji cha Gombani na kwa kweli Mkoroshoni imepakana na uwanja wa michezo wa kimataifa, moja miongoni mwa viwanja bora hapa Tanzania. Uwanja huo hujulikana kwa jina la uwanja wa Gombani. Eneo ulipojengwa uwanja huo huitwa Gombani mpya. Gombani mpya imeibuka kuutofautisha uwanja huu na uwanja wa zamani wa kienyeji ulioitwa Gombani ya kale. Viwanja vyote viwili hadi leo vinatumika. Mashariki ya kijiji cha Mkoroshoni kwa upande wa kusini kuna kijiji cha makaazi ya wenye nacho kiitwacho masikini hajengi. Upande wa kaskazini mashariki ya Mkoroshoni kuna eneo la kilimo liitwalo Kwakatoto. Kwa katoto ni eneo mashuhuri sana kwa kilimo cha mananasi.Magharibi ya Mkoroshoni kuna bonde la Pagali litumikalo zaidi kwa shughuli za kilimo. Kusini ya Mkoroshoni kuna

kijiji cha Mkanjuni. Watu wa Mkoroshoni ni wajasiriamali wa shughuli mchanganyiko. Wapo wakulima, wafanya biashara na wengi wao ni watumishi wa umma.

4.2.22 Kijiji cha Miembeni

Miembeni ndio kitovu cha mji wa Chake. Ni eneo ambalo nembo na alama zote za mji wa Chake zimejikita. Miembeni kwa upande wake wa kaskazini kuna kijiji chengine kilicho kati kati ya mji kiitwacho Misufini. Mashariki ya Miembeni kuna kijiji cha msingini. Magharibi kuna soko kuu la Chakechake, lililopakana na soko jipya la Tibirinzi (Katari). Kusini ya mtaa wa Miembeni kuna kijiji cha Vichungwani. Ni katika mtaawa Miembeni ambapo Hospital kuu ya Chakechake inapatikana. Mahakama kuu ya Pemba iko Miembeni. Soko kuu na kituo kikuu cha magari pia kipo Miembeni. Maduka mengi makubwa ya bidhaa mbali mbali kama nguo, vyombo, vipuri vya magari, viatu na bidhaa nyenginezo ziko kwenye mtaa huu.Ni sehemu ya mjini yenye kuchangamka sana kwa harakati za kijamii wakati wa mchana. Haina wakaazi wengi sana. Wakaazi wake ni wa shughuli mchanganyiko kama walivyo wakaazi wengi wa mjini.

4.2.23 Kijiji cha Konde

Konde ni kijiji kikubwa kinachobeba hadhi ya mji kwa kiasi. Konde iliwahi kuwa makao makuu ya wilaya ya Michewewni na wakati huo jina la wilaya lilikuwa ni wilaya ya Konde. Wakati huo ofisi zote za serikali ya wilaya zilikuwa huko. Makao Makuu ya wilaya ya konde yalihama huko na kuhamishiwa eneo la Micheweni wakati wa utawala wa Aboud Jumbe Mwinyi. Kuanzia wakati huo jina la wilaya

lilibadilika na kuwa wilaya ya Micheweni. Hata hivyo, baadhi ya ofisi za wilaya ya Micheweni hadi leo ziko Konde.

Konde kwa upande wa Mashariki imepakana na kijiji cha Kinowe. Magharibi kuna msitu mkubwa wa hifadhi ya serikali uitwao msitu wa Ngezi. Kaskazini mwa Konde kuna kijiji chenye historia kubwa sana kwa kisiwa cha Pemba, kiitwacho Msuka. Kusini ya Konde kuna kijiji cha Matangatuwani. Watu wa Konde wengi hujishughulisha na biashara na uvuvi.

4.2.24 Kijiji cha Mabaoni

Mabaoni ni kijiji kilichopo njiani kuelekea uwanja wa ndege huko Mfikiwa kisiwani Pemba. Kusini Magogoni imepakata na mtaa wa Mahita, eneo lenye nyumba za askari zilizojengwa enzi zile ambazo Mahita alikuwa ni mkuu wa Polisi Tanzania. Mashariki ya Magogoni ni eneo la uwanja wa ndege wa Pemba ambalo ni sehemu ya hifadhi ya kiwanja hicho. Kaskazin ya Mabaoni kuna kijiji cha Wawi; kijiji kimoja kikubwa na chenye jina katika historia ya kisiwa cha Pemba. Magharibu ya Mabaoni kuna msitu wa uwanda. Mabaoni ni sehemu yenye wakaazi wachache sana na hiyo ni sehemu ambayo makaazi mapya yanaibuka. Watu kutoka maeneo mbali mbali hivi sasa ndiyo wanajenga eneo la makaazi yao hapo.

4.2.25 Kijiji cha Uwandani

Kijiji cha uwandani ni kijiji ambacho kinapatikana katika ukanda wa mashariki wa kisiwa cha Pemba. Uwandani imejitenga upande wa kaskazini mashariki ya mji wa Chakechake. Uwandani ni kijiji kikubwa sana kilichotandawaa eneo refu huko jirani ya ukanda wa pwani ya mashariki. Uwandani imepakana na Vitongoji upande wa

kusini, kaskazini kwa pembe ya magharibi kuna Ole. Mashariki kuna Kware; inayotumika kuzalisha mawe ya kujengea, kokoto na machimbo ya matofali yam awe. Magharibi ya kijiji cha Uwandani kuna mtaa mwengine mkubwa uitwao Vikunguni. Mbali ya kwamba eneo la Uwandani ni kubwa lakini limebeba nyumba chache na idadi ndogo ya watu. Hata hivyo idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kutokana na majengo mapya yanayojengwa huko. Watu wa Uwandani

4.2.26 Kijiji cha Kijiwe Mtu

Kijiwe mtu ni kijiji kidogo kilichoko maeneo ya Ole. Kaskazini kijiji hiki kimepakana na sehemu ya bahari, iitwayo bahari ya mto wa Ole. Kusini ya Kijiwe mtu kuna sehemu ya makaa ya uwandani na Vitongoji. Mashariki ya Kijiwe mtu kuna bahari ya Hindi, ilhali magharibi yake kuna makaa ya Uwandani pia. Kijiwe mtu ni eneo la shamba za mazao na makazi ya watu wachache waliohamia huko kwa shughuli za kilimo.

4.2.27 Kijiji cha Dumbini

Kijiji cha Dumbini kinapatikana maeneo ya Kangagani, wilaya ya Wete, mkoa wa kaskazini Pemba. Ni kijiji kinachopatikana ukanda wa pwani ya mashariki kisiwani Pemba. Kaskazini mwa Dumbini kuna kijiji cha Kangagani, magharibi kuna Uwandani, kusini ni eneo la Makaani, paitwapo Makaa ya vitongoji. Mashariki ya Dumbini ni eneo la bahari ya Hindi. Mazao makubwa yanayositawi Dumbini ni mbaazi, kunde, chooko, ndizi za koroboi na mihogo. Ni eneo lenye rutba, ila mara kwa mara hupigwa na ukame kutokana na umbile lake la uwanda. Wakaazi wake wengi ni wavuvi na wakulima. Idadi ya wakaazi wake si kubwa sana. Inasadikiwa kuishi kaya kama mia moja na ishirini.

4.2.28 Kijiji cha Msingini

Msingini ni miongoni mwa vijiji vinavyopatikana kaika mji wa Chakechake. Kwa kweli kijiji hiki kipo katikati ya mji. Kijiji hiki kimepakana na kijiji cha muharitani kwa upande wa kaskazini, Kusini ya msingini kuna Miembeni, ilhali mashariki ya kijiji hiki kuna kijiji cha Mtoni. Magharibi ya Msingini kuna kijiji cha Chachani, Msufini na Sukita. Msufini ipo magharibi kabisa, ilhali Chachani iko upande wa kaskazini magharibi na Sukita inapatiana kusini mahariki. Msingi ni mjini na idadi ya watu ni kubwa kiasi cha kuzidi kiwango. Wakaazi wake hawapunguwi elfu mbili kwa kukisia. Ni eneo la mjini lenye wakaazi wa shuguli mchanganyiko. Baadhi ya watu wanaishi hapo kwa kukodi ili kurahisisha shughuli zao za utumishi wa uma.

4.2.29 Eneo la Mto Mkuu

Mto Mkuu ni jina la mto mmoja uliokuwa mkubwa sana katika eneo la Mahuduthi Kengeja. Mto huu uko katika eneo la Kengeja Jimbo la kiwani, mkoa wa kusini Pemba. Mto mkuu kwa upande wake wa kaskazini umepakana na mabonde ya mpunga yaitwayo mabonde ya Sipwese. Kusini ya mto mkuu kunapatikana mabonde ya Kivuma. Magharibi ya Mto Mkuu kuna kijiji cha Kidusini. Mashariki Mto Mkuu umepakana na njia kuu inayotkea Kiwani kwenda Kengeja.

4.2.30 Kijiji cha Ziwani

Ziwani ni kijiji kilichopo katika mkoa wa kusini Pemba, Wilaya ya Chakechake, Shehia ya Ziwani, jimbo la Ziwani. Ziwani imepakana na kijiji cha Mchanga wa Kwale kwa upande wa kusini. Kaskazini Ziwani imepakana na kijiji cha Mgogoni, ilhali kwa upande wake wa mashariki imepakana na kijiji cha Jitenge na upande wake wa magharibi Ziwani imepakana na bahari.

4.2.31 Kijiji cha Mtemani

Mtemani ni kijiji kilichopo katika mkoa wa kaskazini Pemba, Wilaya ya Wete, shehia ya Mtemani. Mtemani imepakana na kijiji cha Bubujiko kwa upande wake wa kusini. Kaskazini Mtemani imepakana na kijiji cha Utaani. Upande wa mashariki Mtemani imepakana na kjiji cha Jadida na kwa upande wake wa magharibi imepakana na kjijicha Kipangani. Mtemani iko kati kati ya mji wa Wete, njiani kuelekea kwenye soko kuu la Wete, hospital na bandarini. Mtemani ni mji uliojengwa majumba makubwa mwaka sabiini na sabiini na moja na marehemu mzee Abeid Amani Karume. Majumba hayo huitwa majumba ya maendeleo. Mpaka leo hii majumba hayo yanapatikana na yanatumika kwa makaazi ya raia.

4.2.32 Kijiji cha Misufini

Misufini ni kijiji lichoko katikati ya mji wa Chake chake. Ni kijiji ambacho kina njia ya kuelekea soko kuu la chake chake. Njia hii hupitia sokoni kuelekea mahakamani na Hospitali kuu ya wilaya ya Chakechake. Pembezoni mwa njia hiyo muna maduka mengi ya bidhaa mbalimbali vikiwemo vifaa vya nyumbani. Vifaa hivyo ni kama vyombo vya kupikia, vifaa vya kilimo, vifaa vya michezo, mafuta mazuri na uturi, viatu na hata nguo.Kwa upande wa kusini mtaa wa Misufini umepakana na soko kuu la Chake chake lilioko mtaa wa Miembeni.Kaskazini yaMisufini kuna kijiji cha Tibirinzi. Mashariki kuna Msingini na Magharibi kuna Mtaa wa Tibirinzi pia uliopakana na soko jipya la Katari. Mtaa wa misufini kwa upane wake wa magharibi kuna makaazi ya watu wengi si haba. Wakaazi wa mahali hapo ni zaidi ya kay mia mbili kwa mujibu wa sense ya 2012.

4.2.33 Kijiji cha Ndagoni

Ndagoni ni sehemu mojawapo miongoni mwa sehemu za rasi Mkumbuu. Ni sehemu iliyoingia ndani isiyofikiwa na maji ya bahari. Upande wake wa kusini na kaskazini Ndagoni imepakana na bahari ya hindi. Mashariki yake kuna Wesha na Magharibi liko eneo la Mkumbuu. Ndagoni kwa sasa ni eneo linalokaliwa na watu wengi kiasi. Watu wake wengi ni wakulima na wavuvi. Kina mama wa huko hujishughulisha na kilimo cha mpunga na kupanda mwani.

4.2.34 Kijiji cha Miburani

Miburani ni kijij kilichopo njiani kuelekea Wete, yapata kilomita tatu na nusu kutoka mjini Chakechke. Hiki ni kijiji miongoni mwa vijiji kumi na moja vilivyojenga eneo la Kwale. Vijiji vyengine ni Birikau, Pembeni, Michungwani, Kukuchuni, Kidemeni, Tumbatu, Niapi na vyenginevyo. Kwenye mipaka yake Miburani imepakana na kijiji cha Gombani kwa upande wa kusini. Kaskazini imepakana na kijisitu kidogo karibu na kijiji cha Niapi, mashariki kuna eneo la Mchekeni na magharibi ni eneo la Mavuleni/bonde kubwa litumikalo kwa kilimo cha mpunga. Wakaazi wa Miburani ni watu wanaojishughulisha na shughuli mchanganyiko. Wapo wanaolima, kuna baadhi ni wavuvi, wapo wachache ni watumishi wa Serikali na wengine ni wajasiriamali wanaojitegemea. Kaya zisizopungua mia tatu na hamsini zinapatikana Miburani.

4.2.35 Kijiji cha Michungwani

Michungwani ni kijiji kilichojitenga bila kupakana na eneo lolote linaloishi watu kwa njia ya kukutanika. Ni moja miongoni mwa vijiji kumi na moja vya kwale kama ilivyofafanuliwa kwenye sehemu ya 4.3.34 hapo juu. Mbali ya kupakana na vijipori

na sehemu za mashamba ya watu, tunaweza kuonesha pembozoni mwake kuna vijiji gani kama ifuatavyo:-

Kwa masafa marefu kabisa kuelekea kusini kunaonekana kijiji cha Pondeani. Kaskazini mashariki ya Michungwani yapata kilimita moja hivi kuna kijiji cha Kukuchuni na upande wa kaskazini magharibi kuna kijiji cha Kichuwani. Kidemeni iko mashariki ya Michungwani. Masafa baina ya vijiji viwili hivi ni kama kilomita mbili hivi. Magharibi kuna mikoko inayoelekea kijiji cha Birikau. Michungwani iko kusini mashariki ya Gombani. Watu wa michungwa ni wakulima wanaozalisha mazaom mbalimbalim kutegemeana na misimu ya mvua. Hata hivyo wengi wao ni wavuvi wa aina mbalimbali za uvuvi. Kina mama hujishughulisha sana na kilimo cha mwani.

4.2.36 Kijiji cha Kichungwani

Kichungwani ni moja ya mitaa iliyo kwenye mji wa Chakechake. Mtaa huu upo ndani ya shehia ya Kichumgwani, wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. Kusini ya Kichungwani kuna-Kijiji cha Madungu ya bondeni kuelekea Gogo Mawe, ilhali kaskazini kuna mtaa wa Miembeni. Mashariki ya Kichungwani kuna mtaa wa Afrikana, ilhali magharibi kuna mikoko inayoelekea baharini. Eneo hilo hujulikana kwa jina ka Kopolo. Kichumgwani ina wakaazi wengi kiasi, ukilinganisha na mitaa mingeni jirani. Tofauti hii imejitokeza kwa kuwa Kichungwani si eneo la ofisi na maduka mengi. Majengo mengi yaliyopo hapo ni makaazi ya raia. Shughuli za watu wa Kichungwani ni kilimo na ujasiriamali. Baadhi yao ni watumishi wa uma kama walivyo watu wengine wa mjini.

4.2.37 Kijiji cha Changaweni

Changaweni ni kijij ambacho kiko njiani kotuku mkoani bandarini yapata kilomita mbili kotuku bandarini pwani mkoani. Shehia ya Kijiji hiki inaitwa Changaweni ambayo iko kwenye jimbo la Mkoani, wilaya ya Mkoani, mkoa wa Kusini Pemba. Kwa upande wa kusini Changaweni imepakana na mabonde yenye mikarafuu mingi iliyojaa kwenye eneo hili. Kaskazini kuna kijiji cha Mikweni. Mashariki kuna kijiji kiitwacho kwa Changawe na magharibi kuna kijiji kijulikanacho kwa jina Vichangaraweni. Hili ni eneo lisilokaliwa na watu wengi sana. Lina wakaazi kama mia moja. Wengi wao ni wakulima na baadhi yao ni wavuvi.

4.2.38 Kijiji cha Vilima Vitatu

Vilima vitatu ni eneo lilioko jimbo la Konde, wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Eneo hili hali wakaazi wengi. Wakaazi wake wengi na wafanya biashara. Watu wa Pemba wenye asili ya Waarabu hupatikana kwenye eneo la vilima vitatu. Kwa upande wa mashariki vilma vitatu imepakana na kijiji kimoja kiitwacho Chimba, magharibi kimepakana na Kipange. Kusini yake kuna Matangatuwani, ilhali kaskazini kuna Konde.

4.2.39 Kijiji cha Limani

Limani ni eneo lililo nadani ya wilaya ya Chakechake, mkoa wa kusini Pemba. Kaskazini ya kijiji cha Limani kuna eneo liitwalo Matuleni, kusini kuna kijij cha Matale. Juu zaidi upande wa mashariki kuna eneo la Mitamani. Magharibi kuelekea upande wa bondeni kuna Chanjamjawiri. Sehemu ya limani kuna miti mingi sana ya mikarafuu, zao ambalo linastawi kwa kiwango cha juu kabisa. Idadi ya wakaazi wa

Limani ni wachache mno na wengi wao ni wakulima wa mazo mbalimbali. Baadhi yao ni wavuvi na wachache ni watumishin wa uma.

4.2.40 Kijiji cha Bandari Kuu

Kijiji cha Bandari Kuu kipo kwanye jimbo la Konde. Kijiji kimejitenga mbali kabisa magharibi ya eneo la konde. Upande wa kaskazini Bandari Kuu, imepakana na Msitu wa Ngezi. Magharibi ya Bandari Kuu kuna ghuba ya Mkia wa Ng'ombe. Kusini kuna bahari ya Hindi, si mbali sana na eneo la Gando. Bandari Kuu ni eneo muhimu sana kwa kusafirishia mizigo ya magendo na safari za kupeleka bidhaa nje ya Pemba kwa njia isiyo rasmi.

4.2.41 Kijiji cha Vuma Wimbi

Eneo la Vuma Wimbi Linapatikana kwenye mkoa wa kaskazini Pemba. Kipo wilaya ya Micheweni kwenye jimbo la Konde. Ni eneo la utalii lenye mvuto mkubwa. Ni katika sehemu hii ambapo hoteli ya chini ya bahari inapatikana. Kaskazini ya Vuma Wimbi kuna bahari ya Hindi, kusini yake kuna Msitu wa Ngezi. Msuka iko upande wa mashariki ya Vuma Wimbi, ilhali upande wa magharibi ya Vuma Wimbi kuna bahari ya hindi pia. Vuma Wimbi ni sehemu ya utalii yenye kuchangia pakubwa uchumi wa Taifa. Ni eneo ambalo hoteli iliyochini ya bahari.

4.3 Historia za Kuibuka kwa Majina kutokana na Mazingira ya Kimaumbile

Lengo la pili la utafiti huu kama ilivyobainishwa kwenye ( ) ni kueleza asili na histori ya kuibuka majina ya mahali kutokana na mazingira ya kimaumbile, kisiwani Pemba. Katika sehemu hii mjina yasiyopungua ( ) yamebainishwa na kufafanuliwa

asili na historia ya kuibuka kwake, kama inavyoonekana kwenye 4.3.1 hadi 4.3.41 hapo chini:-

4.3.1 Historia ya Kijiji cha Mivumo Ishirini

Bi Fatma Rashid Moh'd alipoulizwa kwa nini mahali hapa paliitwa Mivumo Ishirini, alsema habari hii ni ya historia. Muvumo ishini lilikuwa ni eneo la konde, lilikuwa si makaazi ya watu kwa wakati huo, lilikwa lina miti iitwayo mivumo, Bi Fatma alisisitiza kwa kujiamini sana. Idadi ya mivumo ilikuwa ni ishirini. Ilikuwa ni ishirini kamili bila kuzidi, wala kupungua, Bi Fatma alisisitiza kwa ufasaha wa hali ya juu. Aliendelea kusema kwamba nadhani kwa sababu hii ndio eneo hili likaitwa Mivumo Ishirini. Maelezo haya Bi Fatma aliyatowa siku ya tarehe 28/05/2018 alipokuwa akihojiana na mtafiti wa kazi hii.

Kwa upande wa mwega wa kinadharia, mtafiti amegundua kwamba kilikuwepo kibainishi kilichopafanya mahali hapa paitwe Mivumo Ishirini. Kibainishi chenyewe ni kule kuwepo idadi hii ya mivumo. Kuhusu kulinda asili na kuhifadhi utamaduni wa kimaumbile lilikuwa ni jambo gumu sana kutokana na maeneo mengi kuathiriwa na shughuli za kibinaadamu. Mivumo hii haipo tena na wala mivumo mingine haikupandwa kuziba pengo lililoachwa. Jambo la kushukuru ni kwamba jina limebaki na linaendelea kutumika hadi sasa.

4.3.2 Historia ya Kijiji cha Kidutani

Mtafiti alimuhoji bwana Bakari Haji Ajabu siku ya tarehe 6/04/2018. Alimuhoji kwa kutumia maswali maalum aliyoyaandaa kwa ajili hiyo. Katika mahojiano hayo bwana Ajab alisema Kidutani ni kijiji kilichoanzishwa na Mzee Makame Haji

Makame katika miaka 1800s: mwishoni mwa karne ya 19. Mzee Makame ni Mtumbatu mzaliwa wa Bumbwini Bwaga. Bumbwini Bwaga iko wilaya ya Kaskazini B, Mkoa wa kaskazini Unguja. Bwana Makame aligundua eneo hili alipokuwa na mazoea ya kuja kisiwani Pemba, kwa lengo la uchumaji wa karafuu. Wakati huo Bwana Makame alikuwa uenyejini pake hapa kisiwani Pemba ni maeneo ya Nanguji huko maeneo ya Kengeja. Eneo hili la Kidutani lilimvutia mno Mzee hayu hasa kwa vile halikuwa na mmiliki rasmi. Wakati huo eneo hili lilikuwa ni pori lililotawaliwa na miti tofauti tofauti. Mzee Makame aliamua kuanzisha makaazi yake na kuanza kuvunja pori lilikuwepo na kuanzisha kilimo cha mikarafuu. Kwa hakika mikarafuu ilinawiri na kustawi sana kutokana na hali ya mazingira ya eneo hili. Mzee Makame aliliita eneo hili kwa jina la Kidutani. Jina la kidutani lililotolewa kutokana na muinuko uliopo na mazingira tulivu yaliochangiwa na kuzungukwa na miti iliyoshikana. Hadi kufikia sasa kidutani ni kijiji chenye wakaazi wapatao tisiini (90) ambao ni mchanganyiko wa wazee na watoto.

Kwa ujumla mazingira ya kimaumbile yaliyokuwepo na yaliyopo hadi sasa yaliyochangia kuibuka kwa jina la kijiji cha Kidutani ni kuwepo kwa kijilima kidogo ambacho kule Pemba huitwa kiduta na kwa hivyo jina la Kidutani likaibuka na kuendelea.

Kwa upande wa matumizi ya nadharia inaonekana kwamba nadharia teule imeakisi jina hili kwa msingi kwamba kuna kibsainishi maalum kilichotumika ili kulipa jina eneo hili.Hii ndiyo hali halisi kwa kuwa nadharia hii hutumika katika utafiti huu wowote kwa sababu huhusisha vibainishi jumuishi kadhaa ambavyo vimetumika kwa pamoja kubainisha majina ya mahali katika jamii husika.Nadharia hii imetumika kwa

kuwa hapa palikuwa kibainishi cha Kiduta kilichofanya mahali hapa paitwe Kidutani. Nadharia hii inaendelea kuonekana kuwa ni yenye kufaa kwa kile kitendo cha kuendelea kukilinda na kukihifadhi Kiduta kilichoasisi jina. Kiduta wenyewe ni kidogo tena ni chenye mchanga mwingi kule mawe hivyo kingeweza kuondosha tu na shughuli za kibinaadamu, ila wakaazi wa hapo wameendelea kukilinda ili kuhifadhi historia. Hili linaenda sambamba na nadharia teule kwa kuwa miongoni mwa vipengele vyake nadharia inasema Nadharia hii inasisitiza kwamba haitoshi tu kutambua na kuthamini vibainishi hivyo jumuishi bali pia kuna haja ya wanajamii lugha wenyewe kuendelea kudumisha kwa vitendo vibainishi hivyo vya msingi ili utambulisho wao uweze kudumu.Kwa jamii ya Wapemba kuendelea kutumia majina ya mahali na kuendelea kuhifadhi baadhi ya vibainishi ni ishara ya kuthamini tamaduni zao, historia na lugha pamoja na umoja wao wa kiudugu.

4.3.3 Historia ya Kijiji cha Bubujiko

Bi Ramla Omar Saleh mkaazi wa Wete na mwalimu mkuu wa Shule ya msingi ya Kizimbani alhojiwa na mtafiti wa kazi hii kuhusiana na asili ya jina Bubujiko kuitwa eneo hili. Mahojiano hayo yalifanyika mwishoni mwa April na mapema Mei. Bi Ramla alimchukua mtafiti wa kazi hii hadi hapo mahali paliposababishwa mtaa huu kuitwa Bubujiko. Mtafiti alishuhudia sehemu hii, Kwa kwelim sehemu hii ni ya ajabu sana. Ni eneo lililokaribu sana na ufukwe wa bahari ya Hindi, sehemu ya magharibi ya Wete. Katika sehemu hii kuna chem-chem ya maji baridi inayotowa maji kwa wingi sana. Sehemu inayotoa maji imenyanyuka kidogo na sehemu inayoelekea pwani iko kibondeni. Maji kwa muktadha huu yanateremka kwa kasi na

kububujika pwani kwa muanguko mkubwa. Muktadha huu umelifanya eneo hili liitwe Bubujiko. Sehemu hii mtafiti kaiona kwa jicho lake mwenyewe.

Nadharia teule imeakisiwa moja kwa moja katika eneo hili. Mtafiti ameshawishika kusema hivyo kwa sababu kibainishi kilichofanya jina hilo liibuke kilikuwepo na hadi hii leo mtafiti anapoandika kinaendelea kuwepo. Pili kibainishi hiki kimehifadhiwa mpaka leo hii na hakijaathiriwa na shughuli za kibinaadam. Muktadha huu unaonesha kwamba nadharia jumuishi ni faafu sana katika kuchambua data iliyokusnywa katika eneo hili.

4.3.4 Historia ya Kijiji cha Mtoni Msengele

Mtoni msengele ni kitongoji kidogo sana ambacho kinakadiriwa kuwa na ukubwa wa nusu kilomita. Wakaazi wa kitongoji hiki ni wahamiaji kutoka katika kijiji jirani cha Msengele. Eneo hili limeitwa mtoni kutokana na tabia yake ya kutuama maji hasa wakati wa mvua kubwa. Watu kotuka msengele walishawishika kuweka makaazi na kuanzisha kilimo cha mpunga. Kwa sasa kitongoji hiki kimekuwa ni makaazi rasmi ya watu na kina jumla ya wakaazi hamsini (50) wazee na watoto. Taarifa hizi zimepatikana kwa njia ya usaili kati ya mtafiti na mzee Salim Habibu Khamis ambae ni mzee wa kijiji cha Mtoni Msengele. Mahojiano kati ya mtafiti na Salim yalifanyika siku ya tarehe (26/4/2018), mtafiti alipotembelea huko kwa ajili ya kutafuta taarifa.

Kwa ujumla mazingira ya kimaumbile yaliyopo hapo na kukipa kijiji hiki jina na Mtoni ni kuwepo kwa mto unaotokana na kutuwama maji mengi siku za mvua. Ili kukitofautisha kijijij hiki na vijiji vyengine vinavyoitwa mtoni, kijji hiki huitwa

Mtoni Msengile. Eneo la bwawa linalokusanya maji mpaka leo linapatikana. Shughuli za kibinaadamu zilizoyaumbua maeneo mengi hadi kufikia kupoteza uasili wake bado hazikuathiri eneo hili. Eneo limeachwa kama zamani, ila pembezoni mwake ndimo mulimofanywa makaazi ya watu. Hali hii inaakisi moja kwa moja nadharia jumuishi iliyoteuliwa. Nadharia hii ina vitu viwili, cha kwanza ili jina la mahali litolewe ni lazima kwanza pawe kibainishi na pili ni wajibu wa jamii husika kukilinda kibainishi chenyewa ili kuhifadhi utamaduni na historia yao. Kuhusu jambo la kwanza kibainishi kilikuwa ni kuwepo mto na kwa kipengele cha pili, mto huu unaendelea kulindwa mpaka leo na unaonyesha jinsi watu wa jamii hii wanavyolinda vibainishi vyao vya asili, hivyo kwenda sambamba na nadharia teule ya ujumuishi.

4.3.5 Historia ya Kijijij cha Jiweni

Siku ya tarehe 24/4/2018, mtafiti wa kazi hii alihojiana na bwana Khamis Kai Khamisi kuhusu historia ya kijiji cha Jiweni. Bwana Kai alisema, Jiweni iliwahi kukaliwa na watu wanaosadikiwa kuwa walitoka Mombasa ya Kenya. Watu hao walifika hapo kwa kutumia vyombo maalum vya usafiri viitwavyo jahazi. Wasafiri hao kwa kweli walivutiwa sana na sehemu hiyo kutokana na mazingira yake mazuri yenye kuvutia na kwa hivyo wakastakimu kwa kitambo kikubwa. Mahali hapo baadae paligeuzwa makaazi ya watu hao ambao walifika kutoka Mombasa. Waliendeleza kazi zilezile walizokuwa wakifanya kwao kabla ya kuhamia eneo hili. Shughuli za watu hawa zilikuwa ni kilimo na uvuvi. Kwa sasa hivi eneo hili halikaliwi na watu na kwa hakika limechukuliwa na serikali na kuingizwa katika hifadhi ya msitu wa Ngezi. Eneo hili lilikuwa na mawe mengi yaliyoshikana na

kushonana mtatabia. Kutokana na wingi huo wa mawe eneo hili lilijipatia jina na Jiweni.

Kwa ujumla eneo hili lilipewa jina la Jiweni kwa sababu ya kuwepo mawe mengi yaliyoshikana na kushonana. Muungano wa mawe hayo kulitoa sura ya eneo lililo na jiwe moja kubwa na kwa hivyo pakapewa jina la Jiweni. Hadi sasa athari hiyo inaonekana kwa uwazi, mbali ya kuwa mawe mengi yameng'olewa kwa shughuli za ujezi wa nyumba za makazi na kuchomwa kwa kutengenezwa chokaa. Kibainishi kilichofanya eneo hili kuitwa Jiweni ilikuwa ni kuwepo mawe mengi yaliyokuwa na sura ya jiwe moja kutokana na kuungana kwa pamoja. Kigezo cha kuwepo kibainishi kinaonesha kuakisiwa na nadharia teule, kigezo cha kukilinda kibainishi wenyewe kimedorora kidogo kutokana na kujitokeza kwa wingi shughuli za kibinaadamu. Mawe yalivunjwa kwa shughuli ya ujenzi na kuchoma chokaa, kwa hivyo nadharia imeakisiwa ingawa si kwa asilimia mia moja.

4.3.6 Historia ya Kijiji cha Ndaambani

Ndaambani ni aina ya majani jamii ya nyasi, mashuhuri kwa kutengenezea majamvi na vikapu. Miti hii inalingana na miyaa au majani ya mivumo na kazi zao zinalingana. Kutokana na historia ya kuwepo ndaamba nyingi eneo hili lilijinyakulia jina la Ndaambani. Miti ya aina hii hadi leo inapatikana ingawa kwa uchache katika eneo hili. Taarifa ya kwamba eneo hili lilikuwa na ndaamba nyingi na ndiyo likaitwa Ndaambani zimetolewa na bwana Juma Wadi mkaazi wa Mkia wa Ng'ombe jirani na eneo la Ndaambani. Nadharia jumuishi iliyoteuliwa inafanya kazi sana na kuakisiwa pa kubwa kwenye kipengele hiki. Mtafiti ameshawishika kusema hivyo kwa sababu miti iitwayo ndaamba ambayo ndiyo iliyofanya eneo hili liitwe kwa jina la

Ndaambani ipo mpaka leo. Kwa muktadha huu kibainishi cha kuita jina kwa kiasi fulani kimeendelea kulindwa. Kwa mnasaba wa nadharia tuliyoitumia kupitia misingi yake tunaona hapana shaka imeakisiwa.

4.3.7 Historia ya Kijiji cha Mchangani

Kama unbavyopaona hapa ni pahali penye mchanga mwingi usio kifani. Nadhani kwa sababu hii ndiyo pakaitwa Mchangani. Maelezo hayo yalitolewa na Mzee Shaame bin Mwadini alipokuwa akihojiwa na mtafiti aliyefika huko tarehe za mwisho za April 2018, kwa aji ya kutafuta taarifa zilizofanya eneo hilo kuitwa Mchangani. Kwa ujumla mahali hapa paliitwa Mchangani kwa kuwa palikuwa mchanga mwingi sana ulio zagaa kwenye ardhi hii. Mpaka leo pia eneo hili lina mchanga mwingi wa hatari.

Kwa upande wa mwega wa nadharia mtafiti anahisi kwamba nadharia aliyoitumia ni yenye kufaa moja kwa moja pasina chembe ya shaka. Mtafiti amepata ujasiri wa kusema haya kwa sababu, mahali hapa pana kibainishi cha wazi cha kuitwa Mchangani. Kibainishi hiki ni kule kuwepo kwa mchanga mwingi kupindukia. Kuhusu kulindwa kwa kibainishi hiki pia ni kitu kinachopatikanwa, ingawa ulinzi wenyewe ulikuwa ni wa kimaumbile kutegemeana na maumbile ya ardhi wenyewe. Mcha upo kama ulivyokuwepo zamani. Kwa muktadha huo mtafiti anathubutu kusema kwamba nadharia teule imekuwa ni faafu sana.

4.3.8 Historia ya Kijiji cha Miti Ulaya

Eneo hili linaloitwa Miti Ulaya ni eneo lililokuwa na miti ya kivuli ambayo hutoa maua kila ufikapo mwezi wa Disemba iitwayo ***'Christmas tree'*** Miti hii ilikuwa ilipandwa kwa wingi katika eneo hili. Miti hii mpaka leo ipo kwenye eneo hilo. Wakazi wa Wete wa wakati huo, waliamini kwamba miti hiyo ilitoka Ulaya, na wakaiita miti ulaya. Mtaa huo kwa hivyo nao ukaitwa mtaa wa Miti ulaya. Jina hilo lilidumu na limeendelea kutumika hadi leo.

Maelezo hayo yanaonesha kwamba, mtaa wa Miti Ulaya umepata jina lake kutokana na kuwepo miti iliyopandwa kwenye mtaa huo, iliyoitwa na wenyeji wa Wete kuwa miti ulaya, kutokana na asili ya miti hiyo. Eneo la Miti Ulaya hivi sasa lmeendelea kuhifadhi numashuhuri wake kwa kuwa pana shule moja kubwa miongoni mwa shule zilizomo katika mji wa Wete. Pia ni eneo ambalo kituo cha walimu cha wilaya ya Wete kinapatikana hapo. Miti hiyo inayoitwa miti Ulaya mpaka leo inapatiaka katika eneo hilo. Taarifa zinazohusu asili na historia hii ni kwa mujibu wa mzee Saidi Salim wa Wete, siku ya tarehe 02/05/2018.

Kwa upande wa mkabala wa matumizi ya nadharia, mtafiti anaona kwamba nadharia jumuishi hapa inafaa kabis, kwa sababu kibainishi kilichofanya eneo hili liitwe Miti Ulaya bado kipo na kimeendelea kuhifadhiwa. Jambo hili limeakisi moja kwa moja nadharia jumuishi iliyoteuliwa kama ilivyobainishwa kwa matakwa yake ya kuzingatia kuwepo kibainishi cha kutoa jina la mahali na kuendelea kukilinda kibainishi wenyewe, kama inavyoelezea wazi wazi nadharia wenyewe. Nadharia inayotumika katika utafiti kwa sababu imehusisha vibainishi jumuishi kadhaa ambavyo vimetumika kwa pamoja kubainisha majina ya mahali katika jamii

yaWapemba.Nadharia hii inahusisha vibainishi vingi vya kijamii ambavyo humtambulisha mzungumzaji.Nadharia hii inasisitiza kwamba haitoshi tu kutambua na kuthamini vibainishi hivyo jumuishi bali pia kuna haja ya wanajamii lugha wenyewe kuendelea kudumisha kwa vitendo vibainishi hivyo vya msingi ili utambulisho wao uweze kudumu.

Kwa msingi wa naharia hii tunaona wzi wazi kwamba ndahari hii ndiyo faafu kwenye uchambuzi huu kwa kuwa vibainishi vilivyotumika kutoa jina hili havikupotezwa bali vimebaki hadi leo hii. Hili linaonesha nadharia jumuishi ndiyo hasa inayofaa kutumika hapa.

4.3.9 Historia ya Kijiji cha Mawe Matatu

Kijiji cha Mawe Matatu kwa muda mrefu hakikukaliwa na watu. Watu wa mwanzo kuhamia kijiji cha Mawe Matatu ni wale waliotoka Mchanga Mdogo na wale waliotoka Kiuyu Mbuyuni. Kilichowavutia wahamiaji hao ni rutba ya hali ya juu iliyopo kwenye ardhi hiyo. Mazao yanayostawi zaidi kwenye eneo hilo ni viazi vitamu na muhogo. Maelezo haya mtafiti wa kazi hii aliyapata kutoka kwa mzee Thani Khamis Juma kwenye mahojiano yaliyofanyika siku ya tartehe 27/04/2018. Mahojiano hayo yalifanyika wakati mtafiti alipofika huko kwa ajili ya kukusanya data za kazi hii. Kuhusu asili ya jina hili, bwana thani alisema, sehemu hii ni ya mawe, inayosemekana kwamba hapo awali ilikuwa na mawe mengi ila palikuwa mawe matatu makubwa sana. Mawe haya ndiyo yaliyolipa eneo hili jina la Mawe Matatu. Mtafiti alibahatika kuona eneo tu ambalo mawe hayo yalikuwepo. Kwa sasa mawe hayo hayapo, yamengolewa kwa shughuli za matumizi ya kibinaadamu. Kwa

ujumla eneo hili lilijipatia jina la Mawe Matatu kutokana na historia ya kuwepo mawe matatu makubwa yaliyokuwepo kwenye eneo hilo.

Nadharia teule kwa kiasi cha asilimia hamsini imeakisiwa na eneo hili kuitwa Mawe Matatu. Kama ilivyodokeza nadharia teule, ili jina la mahali liteuliwe ni lazima pawe vibainishi vinavyoendana na jina lililoteuliwa. Vibainishi hivyo hapo kale wakati wa uteuzi wa jina hilo vilikuwepo. Hata hivyo, vibainishi hivi kwa sasa havipo, vimelazimika kupotea kutokana na shughuli za kibinaadamu. Mantiki hii inaonyesha kwamba nadharia teule haikuakisiwa vyema kwenye sehemu hii ya pili kwa kuwa wanajamii wameshindwa kuvienzi na kuvilinda vibainishi hivi.

4.3.10 Historia ya Kijiji cha Chanjamjawiri

Mtafiti alifanya majadiliano ya kina pamoja na kuchunguza majibu ya dodoso zake alizozigawa kwa watafitiwa wa eneo husika la Chanjamjawiri na mitaa ya jirani yake. Kwa kurejelea vyanzo vyake, mtafiti alibaini kuwa jina la mtaa wa Chanjamjawiri liliibuka kutokana na kuwa ni eneo ambalo alifia ama alikufa mtu aliyejulikana kwa jina la Mjawiri. Kijana huyu wa kiume alikufa katika eneo hilo kutokana na kuwa aliwakimbia Wareno waliovamia nyumbani kwao wakiwa na lengo la kumdhuru yeye na familia yake katika kipindi hicho cha ukoloni wa Kireno (mwanzoni mwa karne ya 19). Watafitiwa wameeleza kuwa, Mjawiri ambae alikuwa mtoto wa Mkamandume alilazimika kuwakimbia Wareno ili kujikinga na shari zao. Katika kukimbia kwake ilifika wakati akachoka na inasemekana akaomba kwa Mwenyezi Mungu amdidimize aridhini ili asije akadhuriwa na Wareno hao. Dua hio ilijibiwa na akadidimizwa katika eneo la uwanda au wengine waliita chanjaa. Hapo alipodidimizwa mwishowe pakaitwa kwa jina la Chanjamjawiri; yaani chanjaa la

Mjawiri. Jina hili linaendelea kutumika hadi leo. Mtafiti wa kazi hii ameonesha picha aliyoichukua maktaba kuonyesha eneo la Chanjamjawiri kabla haljafanywa makaazi ya watu.

Kwa ujmla eneo hili lilitwalo Chanjamjawiri kutokana na historia ya bwana aliyeitwa Mjawiri ambaye anasadikiwa alizama eneo hilo kutokana na dua yake aliyoiomba kwa Mungu.

Kijiji cha Chanjamjawiri kilipewa jina hili kwa sababu ya kuwepo chanjaa alilopotelea mtu mmoja aliyeitwa Mjawiri. Kibainishi kilichofanya mahali hapo paitwe hivyo ni kuwepo kwa hilo chanjaa ambapo Mjawiri baadae alikimbilia na kuzama. Kwa upande wa kuwepo kibainishi nadharia imeakisiwa, ingawa kwa upande wa kuilinda vibainishi teule nadharia haikujikita moja kwa moja kwa kuwa eneo lenyewe limetumiwa kwa makaazi ya binaadamu kwa enzi na zama nyingi zilizopita, hivyo hata ule uchanjaa umeondoka.

Picha 4.11: Inayoonesha Chanjaa la Mjawiri lilivyokuwa hapo awali kabla ya kuwa makaazi ya watu. (Chanzo cha picha hii ni makumbusho ya Utamaduni-Pemba).

4.3.11 Historia ya Kijiji cha Kilimandege

Kilima ndege kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 4.2.11 ni kilima amabacho kipo katikati ya mji wa Wete ambapo njia kuu kutoka bandarini inapata kwenda sehemu mbali mbali za kisiwa cha Pemba. Kilima hiki kimeitwa Kilimandege kwa sababu hapo zamani palikuwa na miti mingi na mikubwa ambapo ndege wa aina mbalimbali walikuwa wakipunga upepo kwenye eneo hilo. Walikuwa wakidondoa wadudu na kufyonza maua kwa ajili ya kujikimu kwa shida ya njaa. Ndege hao walikuwa wakibaki kwenye eneo hilo takriban muda wa mchana mzima. Kwa kuwa eneo hili lilikuwa juu ya Kilima na kwa kuwa palikuwa ni mahali pa mapumziko ya ndege,

jina la Kilimandege lilibuniwa na likadumu kwa muda na dahari na hadi leo linaendelea.

Kilima kilichoitwa Kilimandegr mpaka leo kipo na mmoja miongoni mwa miti mikubwa uliosadikiwa kuwa ndio kivutio cha ndege wengi bado upo.Hii inaonesha wazi kwamba kibainishi cha kupatikana kwa jina la mahali hapa kilikuwepo na hadi sasa kimelindwa na kuhifadhiwa vizuri. Kwa mantiki hii tunaewza kusema kwamba nadharia teule imesibu vizuri na imefaa kuchambua data za utafiti zilizokusanywa. Jambo la msingi alilopokea mtafiti ni kwamba, miti mingine iliyokuwa kivutio cha ndege ukweli ni kwamba imeathiriwa pakubwa na shughuli za kibinaadamu.

4.3.12 Historia ya Kijiji cha Minazini

Kijiji hiki kimejipatia jina lake kutokana uwepo wa minazi mingi ambayo wagema walikuwa wakiitumia kwa kutengenezea kilevi maalum cha aina maalum iyoitwa gongo ya mnazi au kwa ufupi mnazi. Pia baadhi ya watafitiwa wanasema asili ya kijiji hiki ni kutokana na uwepo wa minazi mingi iliyokuwa imestawi na kunawiri sana.Taarifa hizi ni kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa siku ya tarehe 29/4/2018 huko Minazini ambako mtafiti alifika kwa ajili ya kwenda kutafuta taarifa maalum zilizosababisha kijiji hiki kuitwa Minazini. Kwa vyovyoye iwavyo kijiji hiki jina lake llinatokana na uwepo wa minazi mingi katika sehemu hiyo. Minazi hiyo ni sawa kama ilikuwa ikigemwa na kuzalisha gongo au ilikuwepo kwa ajili ya kuvunwa nazi, makuti ya kuezekea na madafu. Eneola minazini ndiyo linaloongoza kwa minazi mingi katika kisiwa cha Pemba, hapo zamani hadi sasa. Ukiona eneo hili na kuambiwa linaitwa minazini utajua bila kuuliza kwa nini eneo hili liliitwa hivyo. Minazi iliyopo ni mingi sana. Watu wa hapo wameendelea kuhifadhi na kuenzi

historia ya eneo lao. Inapopungua minazi huirerjesha kwa kupanda mipya. Kwa kuwa kibainishi kilichotumika kupaita mahalai hapa Minazini ni minazi na mpaka leo pana idadi kubwa ya minazi, mtafiti ameshawishika kusema kwamba nadharia teule imeswibu na imeafiki vyema.

4.3.13 Historia ya kijiji cha Tibirinzi

Tibirinzi ni kijiji kilichokabiliana na eneo la rasi ndogo iliyoko upande wake wa magharibi. Pepo za pwani hupiga moja kwa moja kuukabili mtaa wa Tibirinzi. Siku ya tarehe 30/4/2018 mtafiti aliambiwa na baadhi ya watafitiwa wake kuwawageni waliokuwa wakizuru Pemba hapo za mani walikuwa hukaa sehemu ya juu ya Tibirinzi kujipatia upepo mwanana uliokuwa ukipuliza kotuku pwani. Pepo za pwani kwaKiingereza huitwa sea breezes. Watu waliokuwa wakienda hapo kujistarehesha na pepo hizo walikuwa husema wanaenda kujipatia sea breezes. Kwa hivyo eneo lenyewe likaitwa kwa jina hilo la Sea breezes, ambalo limetoholewa na kuitwa Tibirinzi au Kibirinzi. Zamani Tibirinzi ilikuwa ni sehemu ya bandari kuu ya vyombo vya jadi kama vile mashua, madau, majahazi na vyombo vyengine vya aina hii.

Eneo la Tibrinzi ni eneo muhimu sana kwa shughuli za jamii ya Wapemba na Serikali ya Mapinduzi kwa ujumla. Ikulu ndogo ya mji wa Chake iko Tibirinzi. Soko jipya la kisasa linaloitwa soko la Katari liko Tibirinzi. Soko ya makamu wa pili wa raisi na jengo lililokuwa likitumika kwa ajili ya ofisi ya makamu wa kwanza wa rais liko Tibirinzi. Maduka makubwa mapya yanayouza bidhaa mbalimbali yamejengwa kwa wingi huko Tibirinzi. Kanisa katoliki kubwa sana na la kisasa limejengwa Tibirinzi. Hata benki ya PBZ nayo iko Tibirinzi.

Kwa upande wa mkabala wa kinadharia mtafiti anathubutu kusema kwamba nadharia teule imeakisiwa kiasi cha kutosha. Mtafiti anathubutu kusema hivi kwa sababu kibainishi kilichofanya eneo hili kupewa jina kilikuwepo na mpaka leo kipo. Kibainishi hicho ni pepo za pwani kupiga moja kwa moja na kupuliza kwenye maeneo hayo. Pili eneo hili limehifadhiwa kwa kuwachwa wazi na kuachwa mikoko ya kimaumbile kuendelea kustawi. Kwa hivyo maji ya bahari yanakuja mpaka karibu na soko la Katar na pepo mwanana zinaendelea kupuliza hadi sehemu za juu kama zamani. Kwa ujumla nadaharia teule imesibu na kuakisiwa ipasavyo. Sasa hivi ile bandari mashuhuri iliyokuwa ikitumika enzi za kale sasa haipo tena, lakini eneo la pwani limebaki na limehifadhiwa.

4.3.14 Historia ya Kijij cha Mtoni Chake chake

Mto ni msururu wa maji yanayotembea. Kijiji hiki kilibahatika kupitiwa na mto. Mto huo ullikuwa unatumiwa na wanakijiji kwa shughulu zao mbalimbali kama kufua, kuchota maji, kuosha vyombo na shughuli nyengine mbalimbali. Hivyo watu walipokuwa wanakwenda kuelekea kwenye mto ulipo eneo hilo walisema wanakwenda mtoni. Hatimae jina la kijiji hicho likabakia kuwa Mtoni kutokana na uwepo wa mto katika kijiji hicho. Kwa ujumla kijiji cha mtoni kajipatia jina lake kutokana na eneo hilo kuwepo moto uliokuwa ukitumiwa na wanajamii katika kuchota maji. T aarifa hizi ni kwa mujibu wa bi Mwamini Juma Mjanaheri ambaye amedai kwamba mto huu yeye aliuwahi na kuushuhudia katika hatua zake za mwisho. Kwa sasa umekauka, maana pembezoni mwake mmejaa tele majumba. Bi Mwamini alidai athari za mto huu ndizo zinazoleta mafuriko hapa kijiji cha Mtoni siku za mvua kubwa. Bi Mwamini alihojiwa mwishoni mwa mwezi Mei 2018.

Kuhusiana na mkabala wa kinadharia, mtafiti anathubutu kusema kwamba kwa kiasi fulani nadharia teule imeakisiwa. Hili analizungumza mtafiti kwa kuwa mahali hapo katika enzi za kale palikuwa mto ambao ulifanya mtaa huu upewe jina la Mtoni. Kwa kweli hiki ni kibainishi kilichokuwa wazi na dhahiri kabisa. Kwa upande wa wanajamii kukilinda na kukihifadhi chanzo hili, hili limekosekana kwa sababu ya mabadiliko ya tabia za nchi na shughuli za kibinaadamu. Hata hivyo alama za michirizi kuonesha eneo hili lilikuwa la mto mpaka leo zinapatikana.

4.3.15 Historia ya Mbuyu Mkavu

Mti wa mbuyu huwa na kawaida ya kuzaa mabuyu. Katika eneo hili panapatikana mbuyu mkubwa uliokubuhu kwa upevu. Mbuyu huu upo upande wa mashariki ya kijiji cha Vitongoji. Mbuyu huu kwa kawaida hautoi majani wala mabuyu. Hivyo watu wakauita mbuyu mkavu. Jina hili lilikuja kutokana na tabia ya mbuyu huo kutokuwa huna ishara ya uhai (hauna mabuyu wala majani). Kwa hakika mbuyu huu kwa ujumla haukuwa mkavu, ila ulikuwa hauoneshi alama ya uhai, kwa kukosa kwake kutoa majani na hili ndilo lililolifanya eneo hili kuitwa Mbuyu Mkavu. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa sheha wa Shehia ya Vitongoji alizozitoa mwishoni mwa mei 2018.

Nadharia Jumuishi ya Giles ndiyo nadharai iliyoteuliwa na kutumika katika kuchambuwa data za utafiti huu. Kigezo kikuu cha nadharia hii ni kuwepo kibainishi kinachotumika kutoa jina na mahali. Kibainishi kilichotumika kutoa jina la mahali hapa ni mbuyu unaonekana kuwa na sura ya ukavu. Mbuyu huo hadi leo upo na umehifadhiwa kama kivutio cha utalii kwa hivyo kigezo cha pili cha wanajamii kutunza asili na utamaduni wa maeneo kimepatikana vizuri sana. Kwa msingi huo

mtafiti wa kazi hii anasema pasina chembe ya shaka kwamba nadharia teule imeakisiwa kwa kiwango cha asilimia mia moja kuhusu kupafanya mahali palipoitwa Mbuyu Mkavu paitwe hivyo.

4.3.16 Historia ya Kijiji cha Mvumoni

Asili ya kijiji hiki ni kuwepo na mvumo mkubwa uliokuwa unasadikiwa kuwa ni makaazi ya majini. Pia watafitiwa wengine walisema asili ya kijiji hicho inatokana na kuwepo mivumo mingi. Lakini kwa ujumla mtaa huo umepewa jina la Mvumoni kutokana na kuwepo mti mkubwa ulioitwa mvumo. Aliyasema haya mzee mmoja wa kijijini hapo mwanzoni mwa mwezi wa mei 2018.

Kuhusu mwega wa kinadharia mtafiti anakuja na maelezo yasemayo kwamba mvumo wa asili uliofanya mahali hapa paitwe Mvumoni sasa haupo, ila kwa sababu ya kuwepo miti ya aina hiyo kwenye eneo hili hapamchanganyi msikilizaji anaesikia kwamba mahali hapo panaitwa Mvumoni. Kwa hivyo kwa kuwa kibainishi kilikuwepo na mivumo inaendelea kustawi eneo hili, ingawa ule wa asili umeondoka mtafiti anathubutu kudai kwamba nadharia teule imeakisiwa vizuri.

4.3.17 Historia ya Kijiji cha Mkungupigi

Asili ya kijiji hiki ni tabia ya watu wa hapo kupenda kupigana fimbo na majirani zao. Kulikuwa na mkungu maalum uliokuwa ukitumika kuendesha shughuli hiyo ya ugomvi wa kutumia fimbo, ambazo huku upembani fimba huitwa pigi. Kutokana na muktadha huu watu waliliita eneo hili kuwa ni Mkungupigi likimaanisha mkungu fimbo kutokana na eneo hili kutumika kwa shughuliza kupigana fimbo. Maelezo haya ni kwa mujibu wa Bishara Moh’d aliyehojiwa siku ya tarehe 24/5/2018

Mkungu uliopafanya mahali hapa paitwe Mkungupigi hauko tena ulimwenguni. Hata hivyo wakati hali hapo panaitwa jina hilo mkungu ulikuwepo na ndio uliofanywa kuwa kibainishi cha kutoa jina. Kwa hivyo mtafiti amethubutu usema kwamba nadharia kwa upande mmoja iliakisi vyema. Kuhusu kukihifadhi kibainishi, hilo halikuwezeka kwa sababu ya shughuli za kibinaadamu na kwa hivyo sehemu hiyo kutumika kwa kazi nyengine. Kwa hivyo mtafiti anaona nadharia aliyoitumia imeakisiwa kwa kiasi fulani, ingawa sehemu yake ya pili yaani kuhifadhi vipengele vya utamaduni havikupatikana.

4.3.18 Historia ya Kijiji cha Chaka la Kati

Kuhusu asili na historia ya kijiji hiki, mtafiti amepata mapokezi ya aina mbili. Kwanza mzee Ali Saidi Haji aliyehojiwa mwishoni mwa mwezi wa Aprili 2018 alisema “sehemu hii ilikuwa na msitu mkubwa ulioko baina ya vijiji vya mpakani. Ulikuwa katikati baina ya kijiji cha Makumbini kilichokuwa kaskazini na Maambani iliyokuwa kusini. Kwenye njia hiyo palikuwa kijia chembamba mno kilichowasafirisha watu kutoka Chambani, Mtangani na Ukitini zilizokuwa kusuni yam situ. Msitu huo umejengwa na miti mikubwa ya aina mbalimbali na kuzongwa na miti kama mibungo na mimea mingine iliyolifunika na kuonekana kuwa na sura ya chaka. Kwa sababu lilikuwa katikati baina ya vijiji tulivyotangulia kuvitaja, lilijipatia jina la Chaka la kati.

Kwa upande wa mkabala wa kinadharia, nadharia teule aonavyo mtafiti ni faafu sana na ilikuwa ni yenye kuakisi mazingira yaliyokuwepo wakati ule. Kuwepo kwa kichaka na kuwepo kwake katikati kumeakisi moja kwa moja nadharia hiyo. Chaka hili lilifyekwa yapata miaka mia moja sasa, eneo lake ni makaazi ya watu. Kwa

hivyo kigezo cha kuhifadhi na kuonyesha asili ya eneo kimeondoka na kwa hivyo, nadharia yetu kwa eneo hili haikakisi tena.

4.3.19 Historia ya Kijiji cha Mikarafuu Giza

Kijiji hiki kilitokana na kuwepo kwa mikarafuu mingi sana katika eneo hilo. Katikati ya mikarafuu hiyo palikuwa na njia iliyokuwa ikipitwa na watu kwa ajili ya kwenda kuchuma karafuu. Njia hiyo ilikuwa na kiza kutokana na kutandwa na mikarafuu pande zote. Kutokana na muktadha huu mahali hapo paliitwa Mikarafuu giza kutokana na giza lililopo mahala hapo. Giza hilo lilikuwa likitokana na wingi wa mikarafuu iliyokuwepo mahali hapo. Taarifa hizo ni kwa mujibu. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa Dedesi aliyehojiwa kati kati ya mwezi mei.

Wakati mahali hapa palipoitwa Mikarafuu Giza ni kweli palikuwa na sifa ya giza kali, giza totoro lililosababishwa na wingi wa mikarafuu iliyokuwepo baina ya pande mbili za njia. Kibainishi hiki kwa wakati huo kiliakisi moja kwa moja nadharia teule. Kwa sasa hivi mikarafuu mingi imetoweka na eneo hili haliwezi kuakisi jina la kuitwa Giza. Mabadilko ya tabia za nchi, shughuli za kibinaadamu na kupungua kwa miti ya mikarafuu kumeifanya hali hii isieweze kulindika na kuhifadhika, hivyo kuipunguzia nguvu nadharia iliyoteuliwa kuzichambua data zilizokusanywa.

4.3.20 Historian ya Kijiji cha Mavapacha

Asili ya sehemu hii ni kuwepo mava. Mava ni sehemu inayozikiwa watu (Makaburini). Sehemu hii ina makaburi kwenye pande mbili za njia. Inasemekana kwamba makaburi hayo yalikuwa yakikutana wakati wa usiku na kuwa mava moja. Hivyo sehemu hii ikajibebea jina kutokana na kuwepo mava yaliogawika

kutokana na njia na ndipo pakaitwa Mavapacha. Kwa mujibu wa watafitiwa waliohojiwa katikati ya mwezi mei 2018 mahali hapo pamekuwa pakizikwa watu tangu enzi na Dahari.

Kwa upande wa mkabala wa kinadharia, Inaonekana nadharia iliyoteuliwa ni ya kufaa moja kwa moja. Hii ni kwa sababu mava ya pande mbili za nija iliyofanya mahali hapa paitwe hivyo ipo na inaendelea kunawirika kwa kuwa watu wanaendelea kuzikwa eneo hilo.Kwa hivyo kwa kuzingatia kigezo cha kuwepo kibainishi na kigezo cha kulinda kibainishi, mtafiti anathubutu kusema kwamba nadharia teule imekuwa ni yenye kufaa pasina hata chembe ya shaka.

4.3..21 Historia ya Kijiji cha Mkoroshoni

Kijiji hiki kipo baina ya Gombani na Macho manne. Mkorosho ni miongoni mwa miti inayostawi katika kisiwa cha Pemba. Miti hii huzaa tunda zinazoitwa korosho. Asili ya kijiji hiki inatokana na kuwepo idadi kubwa sana ya mikorosho katika eneo hili. Mikorosho hiyo ilikuwepo zamani kama sehemu ya misitu mingi ilistawi hapo. Hadi leo hii mikorosho mikubwa iliyosalikima kukatwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kibinaadamu inapatikana eneo hilo.

Kwa ujumla jina la Mkoroshoni limetokana na kuwepo miti mingi na mikubwa iliyoitwa mikorosho ambayo ilikuwa ni mashuhuri kustawi na kunawiri katika eneo hilo. Taarifa hizi zilitolewa na mmoja miongoni mwa wakaazi wa hapo alipokuwa akihojiwa siku ya tarehe 31 mei 2018.

Eneo la Mkorosheni tangu enzi na dahari ni kitovu cha kustawi miti iitwayo mikorosho. Ni ukweli usiopingika kwamba mikorosho ya zama zile za nyuma haipo tena, lakini kwa kuwa mikorosho michache bado ipo hakuna atakeshangaa kusikia mahali hapa panaitwa kwa jina la Mkoroshoni. Uhifadhi wa miti ya mikorosho kwenye eneo hili ingawa si wa makusudi lakini kwa kuwa imetokea kuhifadhika na kuendela kustawi, si vibaya hata kidogo kusema kwamba nadharia teule imesibu na inaonekana ndiyo nadharia faafu kutumika kuchambua data zilizokusanywa.

4.3.22 Historia ya Kijiji cha Miembeni

Kijiji hiki kinapatikana katika mji wa Chake Chake ukitokea hoteli ya kitalii ya serekali kwendea steni. Kijiji hiki kimeitwa miembeni kutokana na asili ya kuwepo miembe mingi katika eneo hili. Kwa sasa hivi hakuna tena miembe. Ni sehemu iliyo katikati ya mji wa Chakechake. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa bwana Hamza Sheha aliyehojiwa mwishoni mwa mwezi wa Mei 2018. Hii ni sehemu ambayo soko kuu la Chakechake lipo, mahakama kuu ya Pemba ipo hapo, maduka ya bidhaa kama nguo, viatu, vyombo vya nyumbani na mambo mengine huuzwa miembeni. Soko kuu la mji wa Chakechake na kituo kikuu cha gari za abiria kuelekea maeneo mbalimbali ya Pemba pia hupatikana ndani ya Miembeni. Kwa upande wa mipaka miembeni imepakana na barabara kuu ya kuelekea mkoani kwa upande wa mashariki, kwa lugha nyingine Miembeni kwa upande wa mashariki imepakana na Afrikana. Jumba la benki ya NMB na lile la tume ya uchaguzi liko ndani ya Afrikana mkabala wa Miembeni upande wa mashariki. Magharibi ya miembeni kuna soko la Katar. Kaskazini ya Miembeni kuna mtaa wa Misufini uloko kati kati ya mji wa Chake chake.

Nadharia jumuishi ya Giles inatumika hapa kwa kuwa kihistoria panaelezwa hiyo miembe ilikuwepo, ila hakuna ulinzi na uhifadhi uliofanyika kulinda asili na utamaduni wa asili wa eneo. Kwa muktadha huu mtafiti anakuja na maelezo kwamba kwa kigezo cha kuwepo kibainishi kilichotumika nadharia imesibu na kwa kigezo cha kulinda na kuhifadhi asili nadharia imekengeukwa.

4.3.23 Historia ya Kijiji cha Konde

Konde kiasili ni eneo lililokuwa halikaliwi na watu. Lilikuwa ni pori kubwa kabisa hadi mwanzoni mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Lilianza kutumiwa kwa shughuli za kilimo cha vipando mbalimbali. Lilikuwa ni eneo la mashamba mengi ya watu wa Msuka na Matangatuweni. Shamba kwa lugha ya Kipemba ni huitwa konde. Waliokuwa wakielekea huko kwa ajili ya kilimo walikuwa wakisema wanakwenda kwenye konde au wanaenda kondeni. Kwa muktadha huo eneo hili liliitwa Konde. Kwa maelezo hayo tumekwishajua kwamba mazingira ya kimaumbile yaliyofanya mji wa Konde kuitwa kwa jina hilo ni kuwepo kwa konde za watu wa Msuka na Matangatuwani.

Sasa Konde si konde tena. Ni eneo la makaazi ya watu, tena kwa kweli unaweza kupaita mjini. Huduma zote kubwa za kijamii zipo. Muktadha huu unaonesha kwamba kigezo cha kulinda asili na utamaduni wa mahali hapo kimepotea, hivyo kuipunguzia uwezo nadharia teule.

4.3.24 Historia ya Kijiji cha Mabaoni

Jina la kijiji hiki linatokana na kuwepo kwa miti mingi ambayo ilitumiwa na watu wa kijji hiki hasa maseremala kwa kupasua mbao. Mbao hizo zilitumika

kwa shughuli mbali mbali kama vile kutengenezea vitu vya samani kama meza, vitanda. Nyengine ziliuzwa na nyengine zilijengewa. Hivyo jina la Mabaoni lilitokana na uwepo wa miti mingi ya kupasua mbao katika kijiji hiki.Maelezo haya ni kwa mujibu wa mzee mmoja mkongwe mkaazi wa hapo ambaye alihojiwa mwanzoni mwa mwezi Juni, 2018.

Kwa upande wa mwega wa nadharia, mtafiti anashawishika kusema kwamba nadharia teule imeakisiwa kwa kuwa wakati jina lilipotolewa palikuwa kibainidhi dhahiri ambacho ni miti mikubwa iliyokuwa ikitumika kuchonga mabao. Kwa sasa miti hiyo haipo, eneo lenyewe limekuwa makaazi ya watu. Kibainishi kimeshikana kulindika na kwa hivyo asili na utamaduni pia vimepote. Kwa kigezo hiki nadharia imekosa kuakisiwa. Kwa maneno mengine nadharia imeakisiwa kwenye kigezo cha kuwepo kibainishi, ila kwa kigezo cha kulinda asili iliyokuwepo nadharia imetetereka kidogo.

4.3.25 Historia ya Kijiji cha Uwandani

Uwandani ni eneo tambarare lenye miti midogomidogo ya kutupia. Eneo lenye kustawi nyasi na misitu aina ya vipepe. Mazingira ya kimaumbile ya eneo hili ni ya uwanda tangu enzi na dahari na ndiyo maana likaitwa uwandani. Ni eneo la kilimo cha mazo yenye sifa ya kustawi kwenye ardhi hiyo. Mazao yanayopandwa na kustawi kwa wingi huko ni uwele, kunde, chooko, mbarazi, mahindi na vitu kama hivyo. Baadhi ya maeneo ya uwandani kuna mabonde ya mpunga na hulimwa huko mpunga wa kutegemea mvua. Ni eneo kame ambalo ni rahisi kuathiriwa na juwa, ila lina rutba ya kutosha wakati wa mvua na kipupwe. Kwa ufupi mazingira ya

kimaumbile yaliyolifanya eneo hili kuitwa uwandani ni hali ya uwanda uliokuweko wakati huo na hadi sasa katika siku hizi tunazoishi, athari za kiuwanda zinapatikana.

Nadharia Jumuishi ndio iliyoteuliwa kuzichambua data zilizokusanywa. Mahali hapa paliitwa uwandani kutokana na kibainishi cha uwanda mkubwa ulioenea eneo pana kotuku kusini hadi kaskazini. Uwanda huo mpaka leo upo. Tofauti kubwa iliyopo sasa na wakati huo ni kwamba sasa hivi sehemu kubwa ya uwandani ni makaazi ya watu na yanatumika zaidi kwa shughukli za kibinaadamu kuliko ilivyokuwa ikitumika hapo zamani. Kwa kuwa kigezo kilichotumika kinahusu maumbile ya kudumu mtafiti anathubutu kusema kwamnba kimehifadhika na kwa msingi huu mtafiti amepata ujasiri wa kusema kwamba nadharia yake ilikuwa ni faafu billa chembe ya shaka.

4.3.26 Historia ya Kijiji cha Kijiwe Mtu

Mtafiti alifika kwenye eneo hili la kihistoria na akajionea kwa macho yake lile jiwe lililojitokeza juu lenye sura kamili inayoakisi umbo la mwanadamu. Ni ajabu kubwa iwapo hali hii itatathminiwa kwa uoni wa ndani. Hii ni sehemu ya mashamba ya wakulima na ni makaazi ya watu wachache walioko huko kwa shughuli za kilimo. Kwa ujumla mtafiti anaweza kusema kwamba eneo hili liliitwa Kijiwemtu kwa sababu lina jiwe moja kubwa lililochongeka na kuwa katika sura na picha ya mtu.

Kuhusu mwega wa kinadharia nadharia jumuishi ya Giles inaonekana ni yenye kufaa kabisa. Ni yenye kufaa kwa sababu kibainishi kilichofanya eneo hili kupewa jina lake hili, kilikuwepo na hadi leo kipo. Kinaendelea kuwepo kwa sababu ya mkakati maalum wa kuhifadhi asili hiyo kama vile ambavyo nadharia Jumuishi ya Giles

inavyoelekeza. Kwa muktadha huu mtafiti anajifakharisha kwa kusema kwamba nadharia aliyoieleza mtafiti ni yenye kufaa kabis kabisa.

2.3.27 Historia ya Kijiji cha Dumbini

Kijiji cha Dumbini kimejinyakulia jina lake kwa sababu ya kuwepo vumbi jingi sana katika ardhi yake. Dumbi ina maana ya vumbi kwa wenyeji na wakaazi wa Pemba. Mzee Jadi, alipohojiwa kuhusiana na asili ya jina la Dumbini alisema kwamba "***Dumbini ni Vumbini. Paliitwa hivyo kwa sababu ya kuwepo Vumbi jingi***". Mzee wangu ndiye aliyenambia habari hii bwana Jadi alisisitiza. Mzee Jadi alihojiwa munamo mwezi Juni, 2018.

Kuhusu mwehga wa kinadhari, mtafiti anaona kwamba nadharia Jumuishi ya Giles ni yenye kufaa sana kwani Vumbi lilililifanya eneo hili liitwe Dumbini lipo na limebaki na maumbile hay ohayo hadi sasa, kwa hivyo nadharia teule ni ya kufaa sana.

4.3.28 Historia ya Kijiji cha Msingini

Asili ya kijiji hiki ni kuwepo kwa misingi (Mitaro) mingi ya kupitishia maji machafu yanayotoka majumbani. Maji hayo yalikutanishwa katika misingi iliyochimbwa pande mbili kando kando ya barabara iliyopita katika kijiji hicho. Hivyo kijiji nacho kikajinyakulia jina la Msingini. Misingi hiyo kwa sasa mingi yao imepotea lakini athari za baadhi ya misingi hadi leo zinadhihiri kwa kuwa ipo inapitisha maji taka ya mvua. Kwa ujumla misingi hii ndio iliyosababisha eneo hili kuitwa Msingini.

Nadharia teule inaonekana kusibu na kuafiki uhalisia wa data zilizokusanywa na kuchambuliwa. Mtafiti ameshawishika kusema hili kwa sababu msingi mkubwa uliofanya mahali haop paitwe msingini mpaka leo upo. Kwa sasa hivi msingi huo umejengwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umekuwa wa kisasa na kwa hivyo unahifadhi uasili wa mahali hapa kuitwa msingini. Kwa manti hii jamii imetumia kibainishi cha msingi kupaita mahali hapa msingini na jamii hiyo hiyo imehifadhi historia ya msingi huo ili kuakisi historian a utamaduni wa mahali hapo. Kwa msingi huo nadharia imesibu na kuakisiwa.

4.3.29 Historia ya Eneo la Mto Mkuu

Kama jina linavyojieleza mto mkuu ni mto mmoja mkubwa uliokuweko huko maeneo ya Mahuduthi Kengeja. Mto kuu ulikuwa ukipokea maji yake kutoka kwenye vichirizi na vijito vingi vidogo vidogo. Kwa upande wake Mto Mkuu ulikuwa ukimwaga maji yake baharini. Mto Mkuu mpaka leo upo, ila hauko kwenye hali yake ya asili. Umepunguza eneo lake la kuchukua maji kwa sababu hauna vijichizizi vingi vinavyomwaga maji ndani yake. Eneo hili tangu zamani hadi sasa halikaliwi na watu, ila makaazi ya watu hivi sasa hayako mbali tena kotuku Mto Mkuu. Kwa hivyo kwa mujibu wa bwana Haji Ali Mwiga aliyehojiwa siku ya tarehe 27/05/2018, ineo hili liliitwa Mto Mkuu kwa sababu ya kuweko mto mkubwa kwenye eneo hili.

Kuhusu kiunzi cha nadharia, mtafiti anathubutu kusema kwamba nadharia jumuishi ya Giles iliyoteuliwa ni faafu sana kwa kuwa kibainishi kilichotumika kuita jina kilikuwepo na hadi leo pia kipo. Kibainishi hichoo pia kimelindwa na kimedumu

hadi leo. Kwa mantiki hiyo tunaweza kusema kwamba nadharia iliyoteuliwa ni faafu na inakubalika moja kwa moja.

4.3.30 Historia ya Kijiji cha Ziwani

Mtafiti huku akimnukuu Moh'd (2016) ambaye amesema Kijiji cha Ziwani kimejinyakulia jina lake la Zwani kinatokana na kuwepo ziwa kubwa la maji baridi. Ziwa hili lilikuwa likijulikana kwa jina la ziwa la Mjatangu. Jamii inayoishi hapo ililiita eneo hili kwa jina laZiwani ikimaanisha sehemu ambayo ziwa lipo. Kijiji hiki kimebahatika kuwa na vijiji vingi ambavyo asili yake inatokana na majina ya kigeni. Miongoni mwa vijiji hivyo ni kama vile Basara asili yake niUarabuni. Watu wa mwanzo waliohamia hapo inasemekana kuwa walitoka Basra.Jina la kijiji cha pili kilichopo Ziwani ni Barawa. Barawa asili yake imetokana na wageni waliotoka Tanga sehemu inayoitwa Barawa nao wakaamua kupaita sehemu hiyo Barawa. Vijiji vyengine ni Tehrani asili yake imefananishwa na Irani, Kirwa asili yake inatokana na Kilwa ya Tanzania bara. Bila shaka hivi sasa ziwa halipo tena, kwani mabadiliko ya tabia za nchi na kutanika shughuli za kibinaadamu zimeua sehemu nyingi za mito na maziwa kisiwani Pemba. Hata hivyo maadamu ziwa lilikuwepo na ndiyo lililofanya eneo hili kuitwa Ziwani, mtafiti anathubutu kusema kwamba nadharia teule imeakisiwa kwa kuwa jina lililopewa mahali hapa lilikuwa na kibainishi chake.

4.3.31 Historia ya Kijiji ncha Mtemani

Kwa mujibu wa Zubeir (2015) na Moh'd (2016) katika miaka ya zamani kulikuwa na utawala wa Ufalme. Mfalme mmoja wa jadi ambaye alikuwa anaishi Mtambwe aliamuru watu wake wateme katika eneo lililokuwa na pori kwa ajili ya kilimo. Watu waliotoka Mtambwe kuja katika sehemu hii kwa shughhuli zao za kilimo walipaita

mahali hapo kuwa ni Mtemani wakiwa na maana kwamba ya sehemu iliyofyekewa kwa shughuli tofauti ikiwemo kilimo. Kwa kumuktadha huo, neo hilo liliitwa Mtemani kutokana na kutemwa kwa amri ya mfalme kwa ajili ya kilimo.

Nadharia teule iliakisiwa wakati ule ambapo mahali hapo palikuwa na athari za kutemwa. Mtema uliokuwepo ndio kibainishi kilichotumika kupaita mahali hapa Mtemani. Jambo la kukilinda kibainishi halikuwezekana, kwani mahali hapo palifanywa masikani na kugeuzwa kati kati ya mji wa Wete. Kwa hivyo nadharia teule kwa upande wa kuteua jina kwa kuzingatia kibainishi ilisibu, ila kwa kigezo cha kukilinda kibainifu husika haikusiubu moja kwa moja kwani ongezeko la watu huyageuza maeneo ya mitemani kuwa makazi ya watu na maeneo ya pembezoni mwa miji kuwa sehemu za mji kama ilvyo mtemani kuwa sehemu ya mji wa Wete.

4.3.32 Historia yaKijiji cha Misufini

Kwa mujibu wa mzee Hamza Sheha aliyehojiwa na mtafiti siku ya tarehe 20/04/2018, Misufini ni mahali palipokuwa misufi mingi sana wakati wa enzi za nyuma sana. Yawezekana ni katika enzi za utawala wa Kireno. Sheha aliendelea kusema kwamba huwezi kuamini kwamba eneo hili lilikuwa na misufi mingi kwa sababu hivi sasa lipo kati kati ya mji na kwa kweli ndiyo kitovun cha mji wa Chakechake.

Kwa upande wa mwega wa nadharia teule, mtafiti anaweza kusema nadharia imeakisiwa kwa upande momoja na imekosa uakisi kwa upande wa pili. Imeakisiwa kwa kuwa enzi za utoaji wa jina misufi ilikuwepo,ila kwa kuwa misifu imekatwa na

kupotezwa kabisa kwenye eneo hilo uakisi wa kigezo cha kuhifadhi historian a utamaduni kimekosekana.

4.3.33 Historia ya Kijiji cha Ndagoni

Hili ni eneo linalosemekana lilikuwa na mimea mingi sana inayoitwa ndago. Ndago ni mimea jamii ya nyasi, ambayo hustawi kwa wingi sana kwenye maeneo yasiyokuwa na miti mikubwa. Ni miti inayostawi kwa kiwango cha juu zaidi baada ya kunyesha mvua za masika zilizokuwa zikinyesha kwa wingi sana kisiwani Pemba. Ili kupunguza kustawi kwa mmeya wa ndago mkulima anapaswa kuungoa chini kwa kuchimbua kiasi chake cha chini kabisa. Kwa ujumla eneo hili liliitwa ndagoni kutokana na tabia yake ya kuota kwa wingi sana na kwa ustawi wa hali ya juu mmea ulioitwa ndago.

Kwa upende wa ufaafu wa nadharia mtafiti nadharia teule ilifaaa sana kutumika kwani kibainishi cha eneo hili kuitwa ndagoni kiko wazi sana; ni kuweko kwa gugu mashuhuri liitwalo gugu kwa wingi sana. Mmea huu bado umebaki kuwa ni kero katika konde za watu wa ndagoni kwa hivyo tunathubutu kusema kwamba nadharia teule ni faafu kwa kiwango maridhawa.

4.3.34 Historia yaKijiji cha Miburani

Mibura ni miti fulani yenye magamba inayoota sana kwenye sehemu za rutuba hafifu kisiwani Pemba. Miti hii huwa midogo midogo na mikubwa kiasi. Hutumika sana kwa kukata misuwaki ya kienyeji na hata kujengea baadhi ya wakati, kutegemeana na umadhubuti wa kinachotaka kujengwa na upevu wa mbura unaotumika. Kwa mujibu wa mwalimu Suleimani Omari Kombo aliyehojiwa siku ya tarehe 21/4/2018,

eneo hili liliitwa Mibrani kutokana na kuwepo kwake mibura mingi sana, kabla eneo hilo halijateuliwa kuwa makaazi ya watu. Kwa sasa hivi mibura ipo pembezoni mwa kijiji hiko kuonyesha asili ya miti hii katika eneo hili. Mibura iliyopo sasa hivi ni michanga na haipati fursa ya kupea na kuwa mikubwa kutokana na kutanuka shughuli za kibinaadamu, zinazoongezeka siku hadi siku.

Kwa upande wa mwega wanadharia, nadharia iliyoteuliwa ni yenye kufaa sana kwenye eneo hili. Ni yenye kufaa kwa sababu kibainishi kilichofanya eneo hili liitwe Miburani kilikuwepo na ishara zake hadi leo zipo zinaendelea kushamirisha asili za jina hili na kuhifadhi utamaduni wa mahali hapa. Kwa msingi huo mtafiti anajifakharisha kusema nadharia yake ni yenye kufaa sana.

4.3.35 Historia ya Kijiji cha Michungwani

Suleiman Omar Kombo aliyehojiwa siku ya tarehe 23/04/2018 alisema eneo la michungwani lilikuwa ni eneo lililotumika kuchungia ng'ombe. Watu kutoka kijiji cha Kwachenga na Kichuwani walifika huko kwa ajili ya kuchunga ng'ombe. Wakati huo eneo hilo lilikuwa limejaa tele miti iliyoitwa michungwa. Watu walikuwa wakisema naenda kuchunga ng'ombe wangu Michungwani. Kwa hivyo Kombo anasema yawezekana hili eneo asili ya jina lake ni Machungani au Michungwani. Michungwa iliyokuweko wakati huu siyo michungwa hii ya kawaida; ni machungwa msittu. Kulikuwa na michungwa yenye kuzaa madazi, machungwa makali na micheza kangaja.

Kwa upande wa mwega wa nadharia, kwa mujibu wa mtafitiwa kibainishi kikuu kilichokipa kijiji hicho jina ni kuwepo michungwa, kwa mantiki hiyo mtafiti anakiri

kwamba nadharia teule imefaa kwa kufuata kigezo cha kuwepo kibainishi. Kibainishi hakikuweza kuhifadhika kwa kuwa michungwa takriban yote ilikatwa kwa shughuli za kibinaadamu. Pili michungwa iliyokuweko milikuwa ni michungwa msitu ambayo thamani ya machungwa yake ni duni hivyo ili lazimika kukatw ili kupisha shughuli nyengine za matumizi ya ardhi zichukue nafasi yake. Muktadha huu unaonesha nadharia iliyotumika haikuwa faafu sana kwa kigezo cha kuhifadhi asili ya jina lililotolewa.

4.3.36 Histioria ya Kijiji cha Kichungwani

Kichungwani ni eneo la mji wa Chake Chake, nyuma ya mji huu kwa upande wa kusini. Kichungwani ndio eneo ambalo Hospitali Kuu ya wilaya ya Chake Chake inapatikana hapo. Kwa sasa hivi jumba la kampuni kubwa ya simu ambayo ndiyo inayotumiwa sana na watu wa Pemba na Wazanzibar kwa ujumla pia lipo Vichungwani. Kwa mujibu wa mzee Nahoda Ali, mzee mwenye umri wa miaka sabiini aliyehojiwa mwishoni mwa mei, “Kichungwani ni sehemu iliyokuwa shamba la michungwa”. Kwa bahati mbaya au nzuri michungwa yake ilikuwa haikuwi hata kidogo. Ilikuwa mifupi sana, hivyo eneo hili lkaitwa Kichungwani. Alpoulizwa kwenye mahojiano mtafitiwa kwa nini hapakuitwa vichungwani alisema sababu hiyo haijui, lakini kwa masimulizi ya wazee wake amedai kwamba paliitwa Kichungwani kwa sababu ya kuwepo vichungwa vingi.

Ikiwa madai ya mzee Moh’d ni ya kweli basi nadharia itakuwa imeakisi na ushahidi wa hoja yake pia unaonekana upo. Ushahidi upo kwa msingi kwamba hata michungwa iliyo pembezoni mwa mtaa huu sio mirefu. Inawezekana rutba ya mahali wenyewe si rafiki sana kwa zao la michungwa. Kuhusu kuhifadhi asili ya jina kwa

kuendelea kuhuwisha michungwa katika eneo hilo haiwezekani kwani eneo lenyewe ni katikati ya mji kwa hivi sasa.

4.3.37 Historia yaKijiji cha Changaweni

Changaweni ni kijiji kilichopo kwenye njia inayotoka bandarini Mkoani kuelekea Chakechake mjini, yapata kilomita moja na nusu. Kijiji hiki kimepewa jina la Changaweni kwa kuwa kina vijiwe vingi vidogo vidogo mithili ya kokoto, vilivyotapakaa takribani kwenye eneo lote la kijiji hicho. Vijiwe vya aina hiyo kwa lugha ya kawaida huitwa changarawe au kokoto ndogondogo. Bi Amina Gogo aliyehojiwa siku ya tarehe 5/06/2018 alisema "***lakini hata hivyo kutokana na bezo la mdomo kupenda urahisi wa kutamka Wapemba wa eneo hilo wamejikuta wanapaita mahali hapo kwa jina la Changaweni***". Hadi leo vijiwe vya aina hiyo vinapatikana hapo kuonesha kuakisi nadharia jumuishi ya Giles iliyoteuliwa. Kibainishi cha kuteuliwa kipo na kimedumu hadi leo. Kwa mantiki hiyo mtafiti anasema nadharia ni yenye kufaa pasina chembe ya shaka.

4.3.38 8Historia ya Kijiji cha Vilima Vitatu

Hili ni eneo laKonde lililopewa jina hili kwa sababu ya kuwepo vilima vitatu mfululizo kati kati ya bara bara. Masafa baina ya kilima kimoja na chengine yanalingana sana. Inakadiriwa masafa baina ya kilima hiki na kile ni kama mita kumi. Vilima hivyo viko kwenye barabara inayosafiri kutoka Konde kuelekea Wete, kupitia njia ya Mgogoni na Kinyasini Pemba. Vilima hivi kwa hakika ndivyo vilivyosababisha eneo hili kuitwa eneo la vilima vitatu.Eneo hili mtafiti amekwenda na kuliona kwa macho yake mwenyewe. Kwa upande wa mkabala wa kinadharia, mtafiti anashawishika kusema kwamba nadharia teule imesibu kwa kuwa kibainishi

ni vile vilima vitatu vilivyopo sehemu hiyo. Vilima ingawa vimechongwa kidogo ili kupisha matengenezo ya bara bara, lakini bado vipo na vinaonekana hadi leo. Hii inatilia mkazo nadharia Jumuishi ya Giles inayohitaji kibainishi katika kutoa jina na kulinda kibainishi chenyewe ili kuhifadhi asili na utamaduni.

4.3.39 Historia ya Kijiji cha Limani

Kutoka barabarani Chanjamjawiri yapata kilomita mbili hadi tatu kuna eneo liitwalo Limani. Limani kama jina lake linavyojieleza ni sehemu iliyoko juu kabisa kulinganisha na usawa wa bahari. Mnyanyuko wa Limani haukufanya kilele cha moja kwa moja. Mnyanyuko hufikiwa kwa kupanda taratibu sana kuanzia chini Chanjamjawiri hadi juu mwisho Limani kwa mwendo wa saa mbili kwa matembezi ya kawaida ya matembezi ya miguu. Unyanyukaji huu ndio ulilolifanya eneo hili kuitwa Limani. Kwa lugha nyengine mtafiti anaweza kusema kwamba Limani pameitwa kwa jina hili kutokana na kuwepo mnyanyuko mkubwa ambao wenyewe huiita lima. Siyo lima kubwa kama linavyoitwa, lakini hili ni jina lake. Aliyetoa taarifa hizi ni mwali Nassor Hamad Juma aliyehojiwa Juni Mosi, 2018.

Kuhusu kiunzi cha nadharia kilichoteuliwa, mtafiti anajifakharisha kwa kukiakisi vyema sana. Amekiakisi kwa kuwa kibainishi kilichotolewa kikowazi na kimeendelea kudumu hadi leo. Uhalisia unaonekana na alama ya jina imebakia.

4.3.40 Historia ya Kijiji cha Bandari Kuu

Bandari Kuu ni eneo la maajabu, lililochongeka kama ghuba ya mita kumi tu. Eneo hili kwa kweli ni eneo la nchi kavu liingialo maji mengi sana wakati wa bavua kubwa. Masafa baina ya makaazi ya watu na maji yanapokomea ni kama mita tatu.

Mahali hapo palikuwa pakifikishwa mashua zitokazo pwani kwa lengo la kupakia bidhaa zilizokuwa zikisafirishwa kwa njia ya magendo. Kwa kweli hii ilikuwa ni kama bandari muhimu ya usafirishaji wa bidhaa za aina hii.Historia hii ni kwa mujibu wa mwalimu Nassor Ali Suleiman aliyoitoa tarehe 06/06/2018

Bandari kuu ni bandari ya kimaumbile ambayo mpaka leo imehifadhiwa na kuendelea kutumika mbali na shughulki za kibinaadamu kuongezeka. Muktadha huu unaonesha kwamba nadharia Jumuishi ya Giles iliyoteuliwa ni yenye kufaa kabisa kwa kuwa kibainishi teuliwa kipo na kimeenedlea kulindwa ili kuhifadhi uasili na utamaduni.

4.3.41 Historia ya Eneo la Vuma Wimbi

Kwa kuwa Vuma Wimbi imepakana na Msitu mkubwa wa ngezi, mkabala na mkondo wa upepo kotuku baharini, sauti ya wimbi la maji ya bahari haliwezi kutoka nje na kuchawanyika. Sauti hiyo hujikusanya na mvumo wake huwa mkubwa sana kiasi cha kusikika kilomita kumi kutoka hapo lilipopiga. Mvumo huu husikika zaidi wakati wa usiku na zaidi pale hali ya hewa inapokuwa shwari. Watu wa vijiji hupokea kishindo cha sauti hizi mithili ya mzinga uliopigwa kwenye masafa ya karibu mno. Watu wanaoathirika zaidi ni wale wote waliojirani na Msitu wa Ngezi. Ukubwa huu wa mvumo umepafanya mahali hapa paitwe Vuma Wimbi. Mtafiti alifika na kushuhudia mwenyewe vishindo vya mawimbi vinavyokuwepo hapo hasa wakati wa bavua kuu.

Mvumo huo hadi leo unasikika katika kiwango kilekile. Hii ni kwa sababu Msitu wa Ngezi umeendelea kuhifadhiwa na kuifanya sehemu hii kuyaziba mawimbi ya

bahari. Muktadha huu unakubaliana na nadharia teule, kwa msingi kwamba kibainishi kilichotolewa kipo na kimeendelea kulindwa hadi leo hii. Kwa hivyo nadharia Jumuishi ya Giles ni yenye kufaa sana katika uchambuzi wa data zilizokusanywa.

SURA YA TANO

MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NAMAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo kama ifuatavyo:

5.2 Muhutasari

Utafiti huu ulichunguza **“**Kuchunguza Mchango wa Mazingira ya Kimaumbile katika Kuibua Majina ya Mahali Kisiwani Pemba”. Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ambayo ni: Kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile yanayochangia upatikanaji wa majina ya mahali kisiwani Pemba na Kuchunguza historia ya mazingira ya kimaumbile kuibuka kwa majina ya mahali katika kisiwa cha Pemba.

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba ikihusisha mikoa miwili ambayo ni Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini. Mkoa wa Kusini ulihusisha wilaya zake zote mbili ambazo ni wilaya ya Mkoani na wilaya ya Chake chake. Mkoa wa Kaskazini nao pia ulihusisha wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni. Baadhi ya majina yanayopatikana katika maeneo mbalimbali ya wilaya zilizotajwa hapo juu ndiyo yatakayo husishwa katika ukusanyaji wa data za uwandani. Kwa upande wa wilaya ya Mkoani, utafiti utafanyika katika maeneo mbalimbali kama vile Kidutani, Changaweni na mengi mengineyo. Wilaya ya Chakechake maeneo yatakayofanyiwa utafiti ni Chanjamjawiri, Ndagoni, Uwandani, Mchangani pamoja na Dumbini. Kwa upande wa wilaya yaWete utafiti huu utafanyika katika maeneo kama vile Mtemani, Kilima Ndege na mengi mengineyo.

Kwa upande wa wilaya ya Micheweni utafiti huu utafanyika maeneo kama vile VilimaVitatu, Mawe Matatu na mengineo.

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji, mahojiano na ushuhudiaji. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo pekee. Nadharia iliyotumika katika uchambuzi ni nadharia Jumuishi ni nadharia ya Gile iliyonukuliwa na waandishi tofauti akiwemo Msanjila na wenzake. (2011). Nadharia ya hii inasisitiza utambulisho wa jamii na kuhusisha vibainishi vingi vya kijamii ambavyo humtambulisha mzungumzaji. Msingi wa nadharia hii unazingatia fasili ya jamii lugha inayosema kuwa jamii lugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamii lugha moja ambayo iko tofauti na jamii lugha nyengine. (Msanjila), kutokana na Giles, asili ya mtu ndio inayotoa utambulisho wa mtu.Nadharia hii inasisitiza kwamba haitoshi tu kutambua na kuthamini vibainishi hivyo jumuishi bali pia kuna haja ya wanajamii lugha wenyewe kuendelea kudumisha kwa vitendo vibainishi hivyo vya msingi ili utambulisho wao uweze kudumu.

5.3 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Kuhusu lengo la kwanza la utafiti lililotaka kubainisha majina ya mahali yanayotokana na mazingira ya kimaumbile yanayochangia upatikanaji wa majina ya mahali kisiwani Pemba, mtafiti alibaini kuwa kisiwni Pemba yapo majina mengi yaliyotoka na mazingira ya kimaumbile kisiwni hapa. Mazingira ya kimaumbile yaliyochangia majina hayo ni miti mikubwa, milima, hali ya ardhi, mito, maziwa, shughuli za kibinaadamu kama mava, mabonde, mawe, na maumbile mengine. Kuhusu lengo la pili, mtafiti amegundua asili na historia ya majina hayo, na jinsi

yalivyoibua majina ya mwahali humo. Alibaini shughuli kama uvuvi, usafiri, kilimo, ugomvi, mapumziko, uchotaji maji mitoni na pirika nyengine zilitoa umashuhuri wa mwahali humo na kufanya watu waamue kuyaita majina ya mahali kutegemeana na mazingira ya mahali hapo. Amebaini pia baadhi ya asili changizi zilizoibua majina zimetoweka na nyigine zinalindwa na kuhifadhiwa. Nyengine zimehifadhika kimaumbile na nyengine zimehifadhiwa kwa jitihada maalum za kijamii.

5.4 Hitimisho

Maeneo ya kimaumbile kisiwani hapa yanaonekana mengi zaidi ila yanaathirika mno kutokana na shughula za kibinaadamu.

5.4.1 Mapendekezo ya Tafiti

Mtafiti wa kazi hii anapendekeza kwamba, tafiti nyengine zinazohusu mchango wa mazingira ya kimaumbile katika kuibua majina ya mahali ufanyike kwengineko nje ya kisiwa cha Pemba. Pili katika kupitia kwake kazi tangulizi amebaini kuwa kuna maeneo mengi ya kihistoria yenye majina ya ajabu ajabu, hivyo anapendekeza tafiti zifanywe ili kuchunguza asili ya majina hayo.

MAREJELEO

Abubakar, A. (1998). *Zanzibar hapo Kale***.** Zanzibar: Masomo Bookshop**.**

Adam, J. & Kamuzora, F. (2008). *Reseach Methods for Buisness and Social Sudies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Ali, H. M. (2016). "Maana za Majina ya Watu wa Pemba katika Lugha ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ally, J. & Wenzake (1930). *Nahau-Al-Waadhih*. Cairo: Daaru Maarifa**.**

Babbie, E. (1999). *The basis of social Research*. Belmont: Wodsworth Publishing Company.

BAKIZA (2008).*Utamaduni wa mzanzibari*. Zanzibar: BAKIZA.

BAKIZA (2011). *Makala za Kisemina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed SaidAbdullah*. Zanzibar: BAKIZA.

Best, J. W. & Kahn, J. V. (1993). *Research in Education*. New York: Ally and Bacon**.**

Buberwa, A. (2010). "Inverstigating of Socio linguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-West Tanzania." Unpublished M.A Disertation, Universty of Dar es Salaam.

Cameroon, K. (1961). *English placenames*. London: Oxford University Press.

Chum, H. (1982). *Desturi na Mila zetu*. Arusha: East Africa Puplication Limited.

Cooper, L. (1989). *Language Planing and Social Change*. Cambrige: Cambrige University Press.

Enon, J. C. (1998). *Education Reseach, Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Hyman, R. (1964). *The Nature of Pschological Inquiry, Englewood cliffs*. London: Prentice Hall.

Ingram, W. (2007). *Zanzibar its history and its Peoples.* London: Stac of International.

Kihore, Y.M., Massamba, D. P. B. &. (2008). *Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. (2006)**.** *Proposal and thesis writing*: *Introduction*. Nairobi: Paulines Puplication Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Reseach Methodology*: *Method and Techniques*. New Delhi: Wiley Estern.

Kothari, C. R. (2009). *Reseach methodology: Method and Techniques, Second Revised Edition,* New Delhi: New Age International (P) L.t.d.

Massamba, D.P.B. (2004). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2002). *Nadharia ya lugha ya Kiswahili-1, Kidato cha tano na sita*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Masebo, J. na Nyangwine N. (2006). *Jitayarishe kwa Kiswahili Kidato cha 3 na 4.* Dar es Salaam. The General bodi Sellers ltd.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia kwa Secondary na Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.* Mwanza: Serengeti Educational publishers (T) Ltd.

Mgulu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhon.

Mlacha, S.A. na Hurs K. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI.

Msanjila, Y. P. Kihore, Y.M. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Muzale, H. R. T. (1996). "Linguistic and Social Culture Aspects in Intelacansrine Bantu Names." *Kiswahili. Vol. 61:28-49.*

Muzale, H. R .T. (1998). *Linguistic and Socio-Cultural Aspects in Interlacustrine Bantu Names*. DUP. Dar es Salaam Tanzania.

Omary, C. & Richard, I. A. **(**1966). "Names Personal in social Cultural Context." Journal of the Institute of Swahili Reseach), Vol. 40/2

Opie, C. (2010). *Doing Education Reserch*. London: SAGE.

Pons, M. (1992). **"**Self Motivation For Acadamic Achievement: The Role of Self-Efficacy Beliefs and Personal Goal Setting." *American Educational Research Vol. 16 pp23-35*.

Saluhaya, M. C. (2010). *Kiswahili-1, Nadharia ya lugha*. Dar es Salaam**:** STC Publishers.

Scotsman, P. (2003)**.** *A grammar of Runyambo Language of Tanzania (LOT) Project* University of Dar es Salaam: LOT Publisher grammar Series No.1

Sengo, T. S .Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi***.** Dar es Salaam: AERA.

Sigh, K. (2007). *Qualitative Social Research Methods*. New Delhi: SAGE Publication**.**

Steere, E. (2010). *A Handbook of the Swahili Language*. East Africa Language Committee**.**

Zubeir, S. Z. (2015). **“**Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba kuwa Utambulisho wa Utamaduni wa Wapemba.**”** Tasnifu ya M.A.Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO NA.1: MASWALI YA HOJAJI KWA WATAFITIWA

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti unaohusiana na uchunguzi wa mazingira ya kimaumbile yanavyoibua majina ya mahali kisiwani Pemba.

Mazingira ya kimaumbile ni mazingira ya asili yaliopo au yaliokuwepo katika mahali husika.Mfano: Mawe, Mito, Milima nk.

Unaombwa ujibu maswali haya kwa usahihi kutokana na uwelewa wako, ili usaidie kutoa matokeo yatakayoisaidia jamii.

Maelezo binafsi.

Jina ……..…… Jinsia …….……..

Umri ……..… Elimu ……

Kazi …… Tarehe ……..……

2. Unaishi mtaa gani? ……..

3. Kwa kawaida kila jina la mahali lina historia yake. Toa maelezo mafupi kuhusu mitaa mitatu unayoijua inayotokana na mazingira ya kimaumbile.

i) Jina la Mahala ……

a. Maumbile yanayoonekana au yaliokuwepo ni yepi? .....

b. Historia fupi ya jina hilo ipi? .....

……

……

ii) Jina la mahali ……..……

a)Maumbile yanayoonekana au yaliokuwepo ni yepi? .....

b) Historia fupi ya jina hilo ipi)?……

……

……

iii) Jina la mahali……

a)Maumbile yanayoonekana au yaliokuwepo ni yepi? .....

b) Historia fupi ya jina hilo ni ipi?.....

……

……

KIAMBATISHO NA.2: MUONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA WAZEE WA VIJIJI VYA PEMBA VILIVYOTEULIWA KUTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU.

MADA: Mazingira Ya Kimaumbile Yanavyoibua Majina Ya Mahali Kisiwani Pemba

Mtafiti……..…….. Tarehe……..……

Tunaomba utueleze kwa kifupi.

jina lako ,

umri wako,

kijiji unachoishi

Tunafanya Utafiti kuhusu Mazingira ya kimaumbile Yanavyochangia kuibua majina ya mahali kisiwani Pemba.

Mazingira ya kimaumbile ni mazingira ya asili yaliopo au yaliokuwepo katika mahali husika.Mfano:Mawe,Milima nk.

Tunaomba ushirikiane nasi kwa kutupatia taarifa zifuatazo:

Taja majina kumi ya mahali unayoyajua ambayo yanatokana na mazingira ya kimaumbile.

i)…… (ii)……

iii)…… (iv)……

v)……vi)……..…

vii)……viii)……..…

ix)…… (x)……

2). Kila jina hutolewa kutokana na historia yake.Toa historia fupi ya kila jina ulilolitaja hapo juu

i. ……

……

……

ii. ……

……

……

iii. ……

……

……

iv. ……

……

……

v. ……

……

……

vi. ……

……

……..……

vii. ……

……

……

viii. ……

……

……

ix. ……

……

……

x. ……

……

……

Ahsante kwa ushirikiano wako.